**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**
**IDARA YA MISITU NA UFUGAJI NYUKI**

**MRADI WA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MISITU TANZANIA**
**(TFCMP) IDA CREDIT 3604-TA**

# USHOROBA WA MSITU WA DEREMA: MILIMA YA USAMBARA MASHARIKI

# MPANGO WA KUHAMISHA SHUGHULI ZA KIPATO (MKUSHUKI) KWA WALIOCHUKULIWA MASHAMBA YAO KWA AJILI YA HIFADHI YA UBIOANUWAI KATIKA USHOROBA WA MSITU WA DEREMA

**IMETAYARISHWA KWA MADHUMUNI YA KUOMBEA MSAADA WA KIFEDHA KATIKA BENKI YA DUNIA KWA AJILI YA MALIPO YA FIDIA**

**September 2006**

**RASIMU**

# MPANGO WA UANZISHAJI WA MASHAMBA MAPYA (MKUSHUKI) KWA WALIOCHUKULIWA MASHAMBA YAO KWA AJILI YA HIFADHI YA UBIOANUWAI KATIKA USHOROBA WA MSITU WA DEREMA

## YALIYOMO


**Utangulizi: Usuli ………………………………………………………… 6**

**Mradi Wenyewe ………………………………………………………… 10**

Athari za Mradi
Kupunguza makali ya Athari

**Watu walioathirika …………………………………………………….. 21**

Mitaala ya kijamii-kiuchumi
Utafiti wa Kwanza
Utafiti wa Pili
Watu wa Milimani

**Kiunzi cha Kisheria …………………………………………………… 26**

Sheria ya Tanzania
Mbinu za Tathmini
Sera ya Benki ya Dunia, na kulinganishwa
na Sheria ya Tanzania

**Kuliingiza Tao la Mashariki katika sera ya Benki ya Dunia ………… 30**

**Kuhamishwa katika Ushoroba ………………………………………… 32**

Wajibu wa Kiasasi Tanzania
Kustahiki kulipwa fidia
Tathmini na Ulipaji fidia ya hasara: zoezi la 2002
Tathmini na Ulipaji fidia ya hasara: masharti ya Benki
ya Dunia kuhusu hasara ya upotevu wa mazao na miti
Mchanganuo wa Mahesabu uliorekebishwa kwa
kufuata Kanuni za Benki ya Dunia
Hatua za kurejesha upatikanaji wa mapato

**Ugawaji Ardhi …………………………………………………………… 43**

**Majukumu ya Uongozi ………………………………………………. 47**

Malipo ya fidia
Umiliki wa Ardhi

**RASIMU**

**Ushirikishwaji wa Jamii …………………………………………………** **51**

**Mbinu za Kushughulikia Malalamiko ………………………………** **53**
**Usimamizi na Tathmini ya MKUSHUKI …………………………...** **56**

**Ratiba ya Utekelezaji ……………………..………………………….** **58**

**Bajeti kwa ajili ya Utekelezaji wa MKUSHUKI …….……………….** **59**

*Orodha ya Majedwali*
**Jedwali 1:** Ushoroba wa Derema: Idadi ya watu katika kila kijiji, wakulima walioathirika na Mashamba yaliyochukuliwa **……………………….** **20**
**Jedwali 2:** Viwango vya Riba na Mfumuko wa Bei: 2002-2006 Tanzania **………………………………..** **38**
**Jedwali 3:** Jumla iliyorekebishwa ya malipo ya fidia yanayopaswa kulipwa mwishoni mwa 2006 kwa mazao yote yaliyoorodheshwa kwa kila kijiji (Sh. Tz) **……………………………………** **39**
**Jedwali 4:** Vyanzo vya fedha kwa ajili ya matayarisho na utekelezaji MKUSHUKI **……………………….** **60**
**Jedwali 5:** Bajeti ya utekelezaji wa MKUSHUKI **………….** **61**

*Vielelezo*
**Kielelezo 1:** Hatua za Kuwezesha Umiliki wa Ardhi katika Nyanda za chini kwa Wakulima wa Derema **……** **50**
**Kielelezo 2:** Ratiba ya Utekelezaji wa MKUSHUKI **………….** **58**

*Orodha ya Viambatisho*
**Kiambat. 1a:** Mchanganuo wa mapato wa kila fungu au zao**....** **62**

**Kiambat. 1b:** Mpangilio wa mapato ya mazao Derema: Tathmini ya fidia: mazao ya shambani**.. ………..** **64**

**Kiambat. 2:** Jumla ya malipo ya fidia yaliyorekebishwa kwa mazao yote, kijiji hadi kijiji **……………..…..** **65**

**Kiambat. 3:** Sampuli za orodha ya mazao (kutoka kampuni ya *Proper Consult, 2002***) …………………………** **66**

**Kiambat. 4:** Orodha ya Watu walioombwa kutoa taarifa **……** **67**

**Kiambat. 5:** Ratiba ya Safari za Ushauri **………………………** **69**

## RASIMU

**Ramani 1:** Ushoroba wa Hifadhi ya Mazingira ya Amani na Vijiji vitano vilivyoathirika ……………………… **12**

**RASIMU**

# MPANGO WA KUHAMISHA SHUGHULI ZA KIPATO (MKUSHUKI) KUCHUKUA NAFASI YA MASHAMBA YALIYOCHUKULIWA KWA AJILI YA KUULINDA NA KUUTANGAZA RASMI USHOROBA KUWA MALI YA TAIFA

Kati kati ya mwaka 2002, wakulima 1128 waliokuwa wakiishi sehemu ya kaskazini mashariki ya Tanzania, kwenye miteremko mikali ya milima ya Usambara Mashariki, waliambiwa kwamba mazao katika mashamba yao madogomadogo katika misitu, nje ya vijiji vyao ilibidi yafyekwe ili kuihifadhi misitu hiyo. “Ushoroba Mpya wa Derema” utakuwa ni kiungo kati ya hifadhi mbili za misitu ambayo inalindwa na mwendelezo wa makazi ya mamia ya ndege, wanyama watambaao, wadudu, spishi za wadudu na mimea ambayo ni adimu sana, na mingine ambayo inatishiwa kutoweka. Wakulima walilipwa fidia ya mazao ambayo yalikuwa katika mpaka wenye upana wa mita tatu kuzunguka ushoroba; mpaka ambao uliwekwa kwa kufyeka mimea iliyokuwa katika mpaka huo. Mazao yao ndani mpaka –yenye thamani kubwa, yale ya iliki, mdalasini, karafuu na pilipili manga, pamoja na baadhi ya miti ya matunda – yalihesabiwa na kuorodheshwa kwa ajili ya kulipiwa fidia baadaye.

Wakulima wakaacha kuyatunza mazao yao. Hata hivyo, fedha iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya kulipia fidia ilikuwa kidogo sana kuliko iliyohitajika. Mnamo mwka 2004 mamlaka husika ya Tanzania ikaiomba Benki ya Dunia kusaidia kulipia sehemu kubwa ya fedha ya fidia. Hatimaye katika mwaka 2006 serikali ikaamua kupeleka maombi rasmi kutengewa fedha katika mradi wa misitu unaofadhiliwa na Benki ili kupata bakaa ya fedha ya fidia iliyokuwa ikitakikana.

Mpango wa Kuhamisha Shughuli za Kipato (MKUSHUKI) unatoa taarifa kamili ya suala hili, na ndiyo hati ya msingi inayotumiwa na Benki kutolea maamuzi yake. Suala hili limetokezea kuwa changamani sana, na wala si suala la kujaziliza kiasi cha fedha kinachokoseakana tu.

# RASIMU

**Utangulizi: Usuli**

**1**. Milima ya Usambara Mashariki ni sehemu ya Tao la Mashariki la milima iliyojitenga ya kusini mashariki kisha ikaelekea kusini kutoka Mlima Kilimanjaro kaskazini mwa Tanzania. Kuanzia mwishonimwishoni mwa miaka ya 1980 Wizara ya Tanzania ya Maliasili na Utalii imechukua hatua za kuilinda na kuifanya mali ya hifadhi Milima ya Tao la Mashariki kutokana na thamani kubwa ya ubioanuwai wake, thamani yake ya hali za hewa zinazoleta mvua ambazo ni chanzo kizuri cha bidhaa za kilimo za hali ya juu na uweza wake wa kuongeza vyanzo vya utalii wa kiekolojia.

**2**. Kwa miongo mingi Milima ya Usambara Mashariki ilikuwa ikichukuliwa na kutazamwa kwa sura na sera tafautitafauti. Katika mfululizo wa vipindi kadhaa kukawa na kilimo cha kahawa kwenye miteremko ya milima, ukataji mbao, na kilimo cha chai; kuchukuliwa kwa sehemu fulani fulani za msitu kama hifadhi za taifa; na kushawishika kwa wakazi wa maeneo hayo kuishi maisha maalumu kutokana na sifa za pekee za tabia ya nchi  na ekolojia ya eneo lao.

**3.** Kipindi cha sasa ambacho serikali imeazimia kushughulikia masuala ya hifadhi kimeshuhudia mwendelezo wa jitihada za kuiweka wazi mipaka ya misitu ambayo tayari imekwishatangazwa rasmi kuwa mali ya taifa, kuongeza misitu mingine mipya kwenye misitu ambayo tayari inalindwa, na kuboresha usimamizi wa kisayansi wa rasilimali za ubioanuwai katika misitu. Kwa kutumia msaada kutoka Serikali ya Ufini tangu miaka ya 1980 pamoja na misaada midogo midogo kutoka katika mashirika ya kimataifa na ya humu humu Tanzania, yajishughulishayo na mazingira, Milima ya Usambara Mashariki imetokezea kuwa mojawapo ya hazina za asili adhimu kabisa katika nchi. Ina kiwango kikubwa sana cha spishi za aina mbalimbali za miti na wanyama kwa eneo kuliko sehemu nyingine yoyote ulimwenguni. Ikiwa imechaguliwa na Programu ya Binaadamu na Anga kuwa sehemu ambayo inapaswa kupewa ulinzi wa hali ya juu kabisa, na kisha ikapata msaada, katika miaka ya mwanzomwanzo ya muongo huu, kutoka Mfuko wa Utandawazi wa Mazingira (GEF), Milima ya Usambara ni sehemu kiini kabisa ya programu, pana zaidi, ya Tao la Mashariki . Kituo cha Hifadhi ya Mazingira cha Amani (HIMAA)

kilichoanzishwa mnamo mwaka 1997, baada ya mipango ya muda mrefu, ndicho kitovu cha juhudi zote za hifadhi. Kikiwa na hekta 8329 (ikiwa ni pamoja na eneo la ardhi ambalo ni shamba la chai ambalo liko chini ya mkataba wa uangilizi chini ya HIMAA), HIMAA ndio ukanda mkubwa kabisa wa misitu ulio chini ya usimamizi wa pamoja katika Tao la Mashariki, na kuchukuliwa kwake kuwa hifadhi ya mazingira (ya kwanza katika nchi nzima), kunakipa dhima maalumu katika shughuli za kitaifa za hifadhi.

**4** Sehemu muhimu kabisa katika mipango ya hifadhi ya Milima ya Usamabara ni kule kuungwanishwa, taratibu, kwa kiasi cha hifadhi za misitu ipatayo kama ishirini na mine, iliyotengana katika milima, na nyanda za chini zinazoelekeana nayo, yote ikiwa na ukubwa wa hekta 32,352. HIMAA tayari imekwisha jumuisha misitu sita, ambayo hapo awali ilikuwa hifadhi ya misitu iliyokuwa inajitegemea, na kupata ukubwa wa hekta 7265 au asilimia 22 ya eneo lote. Kwamba sehemu hizi za misitu ni hifadhi mbalimbali zilizotengana inadhihirisha mmeguko, katika vipandevipande, wa msitu ambao hapo awali ulikuwa ni mwendelezo wa ukanda mmoja wa msitu uliokuwa umeifunika milima hiyo. Mwendelezo huo unakatizwa na sehemu sehemu zinazokaliwa na watu kwenye mabonde na barabara za milima; na maeneo yaliyotengwa kwa kilimo cha chai na misitu ya biashara. Kutokana na kuongezeka kwa mmeguko wa misitu ubioanuwai unapotea. Hii haiwi tu kupunguza, kwa kiasi kikubwa, idadi ya wanyama na mimea katika maeneo yanayopotea, bali pia inapunguza ubioanuwai wenyewe, katika idadi ya spishi mbalimbali zilizomo katika misitu; hii ni kwa mujibu wa nadharia ya kiekolojia na uchunguzi wa muda mrefu uliofanywa na wataalamu wa kisayansi katika misitu hii. Kadri muda unavyopita shinikizo zaidi juu ya spishi hizo[1] na kupotea kwake kunaweza kuharibu kabisa urari wa kiekolojia katika eneo-bio hili lilo adimu. Kwa hiyo Programu ya muda mrefu ya kujaribu kuufufua mwendelezo wa msitu kadri inavyowezekana, inahusiana moja kwa moja na utunzaji wa ubioanuwai.

[1] Katika Tao la Mashariki mnapatikana wanyama wenye uti wa mgongo wapatao 35 (ambao hawapatikani kwingineko nje ya misitu hii) na spishi nyingine 42 zinazopatikana katika Tao na maeneo jirani. Katika Milima ya Usambara mnapatikana pia wanyama adimu sana wenye uti wa mgongo 4, maarufu kabisa akiwa “Urujuani wa Afrika” (*Saintpaulias spp.*). Hapa pia ndicho chanzo cha mimea ipandwayo katika vyungu, ambayo hujulikana sana kama maua ya nyumbani.

**5.** Nyongeza ya kwanza kwenye msitu itakayofanywa ni ushoroba wa Derema. Ukiwa na hekta 790 utatunza eneo la msitu ambalo limekuwa linatoweka taratibu kati ya HIMAA na eneo jingine litakalochukuliwa rasmi, kaskazini, Longuza (kaskazini). Takribani Derema yote ni msitu, asilimia 60 ikiwa kwenye vilima vyenye miteremko mikali na asilimia nyingine kwenye miteremko ya nyanda za chini, chini ya altitudi ya m 850. Kwa pamoja Derema na Longuza zinaongeza hekta 2643 kwenye HIMAA, na kupanua eneo la mwendelezo wa msitu kwa theluthi moja.

**6.** Kwa sasa hivi Derema haijatangazwa rasmi kuwa hifadhi ya msitu wa taifa lakini ni mali isiyo rasmi ("hifadhi ya msitu wa umma") ya vijiji vilivyo pembizoni mwake (taz. ramani ukurasa wa 12). Takribani sehemu yake yote (asilimia 86) iliainishwa[2] kama "kilimo ndani ya msitu" na mtafiti wa zamani K. Hyytiäinen. Uainishaji huo una maana kwamba uoto unaofunika misiti umehifadhika lakini picha za angani, za wakati huo zilizopo, ambazo si sahihi sana, zilionyesha kilimo cha mazao cha hapa na pale chini ya miavuli ya miti. Haina maana kwamba sehemu yote chini ya miti ya misitu imejaa mazao; na kwa hakika upandaji miti na mazao mengine ya mwaka katika msitu ulitawanyika hapa na pale msituni, ingawa kiasi kikubwa kilikuwa karibu na vijiji vidogo (small hamlets) nje kidogo tu ya eneo la msitu (maeneo ya makazi hayakujumuishwa katika hesabu za msituni). Msitu wa Derema uko nyuma ya vijiji na huko ndiko wamekuwa wakipata kuni na bidhaa nyingine zisizo za mbao.

**7.** Ni muhimu kutambua kwamba hali za maisha ya watu wa Milima ya Usambara zimekuwa zikitawaliwa na kubadilikabadilika kwa mambo ya kisera ambayo yamekuwa yakifanywa nje ya maisha ya vijiji hivyo. Katika kipindi cha Wajerumani, kuanzia miaka ya 1890 hadi Vita vya Kwanza vya Dunia, kulikuwa na matumizi makubwa sana ya misitu ya Usambara, lakini wakati huo huo wenyeji wa maeneo hayo hawakuruhusiwa kutumia raslimali yoyote ya misitu hiyo. Maeneo makubwa ya ardhi yalichukuliwa kwa

[2] Data hii na nyingine humu kuhusu majina na ukubwa wa hifadhi na maeneo yake zimechukuliwa kutoka Stig Johansson na Richard Sunday, *Protected Areas and Public Lands: Land Use in the Usambara Mountains* (Maeneo Yaliyozuiliwa naArdhi ya Umma: Matumizi ya Ardhi katika Milima ya Usambara) *Technical Paper 28* ya mradi wa *East Usambara Catchment Forest Project,* Idara ya Misitu na Ufugaji Nyuki na *Finish Forest and Park Service,* na *National Soil Service, Dar es Salaam* na *Vantaa*, 1996. Maeneo na asilimia ni makadirio ya kuaminika kutokana na mazoezi mbalimbali ya upimaji ramani mwanzoni mwanzoni mwa 1990; hakuna makadirio mengi yaliyo makini sana katika upimaji wa siku hizi.

ajili ya kilimo cha kahawa. Baadaye maeneo haya yakabadilishwa na kutumiwa kwa kilimo cha chai, kule kwenye altitudi za juu, na mashamba ya mkonge katika nyanda za chini. Reli ya kutoka Tanga kwenda kwenye milima ya Usambara ikatumiwa kusafirishia mbao; na ukataji huo wa miti na kuacha uwazi ukaanza kuleta mmeguko wa mapema wa misitu iliyobaki. Ukataji, na baadaye upandaji, miti vikatoa fursa za ajira, na watu kutoka nje ya maeneo hayo wakaja katika nchi ya wenyeji, Washambaa (au Shambara, neno ambalo kutokana nalo likapatikana Usambara, yaani mahali pa Washambaa), milimani na katika maeneo ya nyanda za chini yaliyozunguka milima ambako Wabondei, ambao wanahusiana nao, walikuwa wakiishi. Kubadilisha maeneo ya mbao na mashamba ya kahawa na kuyafanya mashamba ya chai na mkonge kukaleta fursa tele za ajira huko milimani; ingawa inaelekea kwamba Washambaa hawakupendelea sana kufanya kazi hizi ambazo zilikuwa na malipo kidogo sana. Biashara ya mbao, na baadaye juhudi za baadaye za kujaribu kunusu mabaki ya misitu, vilisababisha kuondolewa kwa wanavijiji katika baadhi ya maeneo au kuzuiwa kupata mahitaji yoyote kutoka misituni, mara nyingi pasi na kuwepo fidia yoyote. Programu ya Vijiji vya Ujamaa katika Tanzania mnamo miaka ya mwishoni mwa 1960 iliwakusanya watu katika kaya, na wakati huohuo kushuka kwa tasniya mbalimbali katika kipindi hicho (mahuruji (bidhaanje) yakashuka kwa kiwango cha asilimia 90, toka tani 200,000 kwa mwaka hadi tani 20,000 kwa mwaka), kukapunguza kwa kiasi kikubwa sana ajira za kulipwa katika eneo lote. Bustani ya mimea na miche vilivyoanzishwa mwanzoni kabisa na Wajerumani mwaka 1902, katika jitihada za kurejesha uotaji miti, viliifanya serikali, katika miaka ya 1980, iwashawishi watu kulima mazao ya viungo vyenye thamani kubwa. Hivyo, basi mazao hayo yakaenea kwa haraka katika misitu. Iliki, zao lenye thamani kubwa zaidi, hustawi tu katika sehemu zenye unyevunyevu na zenye vivuli vya misitu. Pilipili manga, huota kwa kutambaa kwenye miti yenye vivuli, ambapo karafuu huota ama katika vijiji au misitu. Zao la mdalasini ni nadra sana kupatikana vijijini. Kuanzia miaka ya 1970 viungo hivi vine vya thamani kubwa (haikuruhusiwa kutoa karafuu Zanzibar, lakini hata hivyo ilianza kupandwa) vikaleta nguvu mpya katika mapato ya miji ya watu katika Milima ya Usambara Mashariki. Masuala ya hifadhi ya mazingira yalipozidi kuonekana muhimu sana, wanavijiji wakawa tena wenye kuathiriwa na mabadiliko ya sera, kuendelea kudorora kwa ubioanuwai wa asili wa misituni lilipoanza kuwa suala la kuangaliwa kwa

makini sana katika sehemu hiyo. Mwisho, katika miaka ya mwanzoni mwa 2000, uanzishaji wa miji kote Tanzania, vuvumko jipya la matumizi ya mkonge kama nyuzi asilia (na ubiofueli), na kuongezeka thamani nyanda za chini zilizo jirani, kwa ajili ya kilimo cha matunda mapya, njugu na mazao ya chakula, vyote vinaleta vivutio vipya kwa familia za Usambara; wakati huu wakiwa sasa wanafikiria kuelekeza shughuli zao za uchumi mbali na milima. Kwa ufupi, familia za vijiji hivi zimekuwa na historia ya kukumbwa na mabadiliko makubwa ya mara kwa mara katika shughuli zao za kujipatia riziki; kiasi kwamba wamefikia mahali pa kuona kwamba kila baada ya miaka kama ishirini hivi mabadiliko katika mielekeo ya uchumi au sera vinawalazimisha kuangalia upya mbinu zao za kujikimu kimaisha. Wakulima kulazimishwa kuacha mazao yao ya viungo katika mashamba ya misituni, na ambayo yalikuwa yanawaingizia kipato kizuri, ni mojawapo ya mabadiliko ya hivi karibuni.

**Mradi Wenyewe**

**8.** Mradi wa Hifadhi na Usimamizi wa Misitu Tanzania ulipitishwa mnano mwezi Februari 2001, na ulianza rasmi mnamo mwezi Mei, 2002. Mradi huu ulichukua nafasi ya mradi wa sekta ya misitu uliokuwa unafadhiliwa na IDA. Mradi wa pamoja kati ya Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Tao la Mashariki na Mradi wa Usimamizi ulipitishwa mnamo mwezi Julai 2003 na ukaanza rasmi Mei 2005. Malengo ya jumla ya miradi hiyo miwili yalikuwa:

(i) Kuimarisha uwezo wa Tanzania katika kuratibu na kuongoza shughuli za kuhifadhi ubioanuwai wa misitu.

(ii) Kusaidia uanzishwaji wa mradi shirikishi wa majaribio katika eneo la hifadhi lililochaguliwa ili kuweza kupata matokeo endelevu kuhusu ubioanuwai na maendeleo ya binadamu.


(iii) Kuboresha mbinu na uwezo wa kiasasi wa kushughulikia hifadhi ya ubioanuwai wa misitu, na

(iv) Kuanzisha na kutekeleza, kwa njia ya majaribio, mbinu endelevu za upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za Hifadhi katika Misitu ya Tao la Mashariki.

**9.** Hakuna shughuli yoyote, katika miradi yote miwili inayofadhiliwa na Benki, ambayo inawekeza moja kwa moja katika ulinzi na upanuzi wa Hifadhi ya Mazingira ya Amani (HIMAA), au hata kwa ujumla zaidi, katika shughuli za misitu yenyewe ya milima ya Usambara. Mradi mpana zaidi wa Misitu, unaofadhiliwa na IDA, una shughuli ambazo zinasaidia kuanzishwa kwa Huduma ya Misitu Tanzania, na kuboresha uwezo wa usimamizi wa misitu na mapori; kuimarisha misaada ya usimamizi bora zaidi wa mashamba ya misitu na mapori; kusaidia kuboresha taratibu za usimamiaji endelevu na mikakati ya kifedha kwa ajili ya hifadhi ya Tao la Mashariki. Hakuna uwekezaji wa moja kwa moja katika misitu. Mradi wa Tao la Mashariki, unaofadhiliwa na GEF kupitia Benki, hutoa misaada kwa ajili ya kufanya mabadiliko, katika asasi, kuhusu hifadhi ya ubioanuwai katika misitu, na husaidia katika uanzishwaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Milima ya Tao la Mashariki (Eastern Arc Mountains Conservation Endowment Fund) kwa kutoa kianzio cha dola milioni 7. Shughuli za aina hiyo za mradi wa GEF unaoendeshwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP) huchangia katika Mkakati wa Pamoja wa Hifadhi ya Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki, na shughuli nyingine za hifadhi ya misitu katika jamii za Milima ya Uluguru kusini mwa Milima ya Usambara. Wafadhili wengine wanatoa fedha kwa ajili ya walinzi wa misitu katika Milima ya Usambara Mashariki na kwa ajili ya shughuli anuwai za uzalishaji/kujipatia riziki katika vijiji vya milimani lakini hawatoa msaada wa kugharamia moja kwa moja upanuzi wa HIMAA kwani ufadhili wa Ufini (DIDC) katika milima ya Usambara Mashariki ulikoma 2003

**10** Mpango wa kupanua eneo la hifadhi uliwezekana chini ya ufadhili wa awamu tatu uliotolewa na Ufini kwa Mradi wa Deltao ya Misitu ya Milima ya Usambara Mashariki (baadaye ulijulikana kama Mradi wa Usimamizi wa Deltao ya Milima ya Usambara) (East Usambara Catchment Management Forestry Project (EUCFP), later The East Usambara’s Catchment Management Project (EUCAMP). Watafiti na mameneja misitu kwa pamoja wakatayarisha orodha, ramani na vigezo vya kisayansi kuhusu dhana ya kuacha shoroba za kiekolojia za kuunganisha hifadhi mbalimbali; na hivyo basi kupanua eneo lenye kulindwa muda wote. Mradi wa EUCAMP pia uligharamia ufyekaji uwekaji mipaka ya Derema na kufanya tathmini ya mazao yaliyotakiwa kuondolewa katika ushoroba huo.

## RASIMU




**RAMANI 1**: **HIFADHI YA MAZINGIRA, USHOROBA WA DEREMA, NA VIJIJI VITANO JIRANI VILIVYOTHIRIKA**

1 = KISIWANI  2 = MSASA IBC  3 = KWEZITU  4 = KWEMDIMU  5 = KAMBAI

11. Ili kuweza kuelewa matatizo ya mchakato wa ulipaji fidia ya mazao katika ushoroba wa Derema, kuna haja ya kuurejea mchakato uliotumika kulipia fidia ya mazao yaliyofyekwa wakati mpaka wa ushoroba ulipowekwa. Chini ya msaada wa Ufini hakuna vigezo vya kimataifa vya ulipaji fidia vilivyotumika, pamoja na Ufini yenyewe kufuata kikamilifu maelekezo ya OECD kuhusu uhamishaji watu na ulipaji wa fidia, ambayo yamekuwa yakitumika tangu 1991. Badala yake hapa, sheria ya Tanzania ndiyo ilitumika.

**12**. Mapema mwaka 2001, kwa kutumia mipango iliyokubaliwa na EUCAMP, mipaka ya Ushoroba w Derema ilipimwa. Mpaka uliopimwa ulikuwa na urefu wa kilomita 27.226 na eneo lililozungukwa lilikuwa ni hekta 956.34. Mnamo mwezi Septemba, mazao yaliyokuwa katika upana wa mita tatu za mpaka yalihesabiwa na kufyekwa. Kwa hesabu ya kila zao (mazao yote ya viungo na matunda) kati ya hekta 8.1 zilizofyekwa 92.5% ilikuwa ni mimea ya iliki, na 6.5% ilikuwa ni migomba. Karibu wakati huohuo likatokea tatizo kuhusu njia ya kutumia katika kutayarisha mahesabu ya malipo ya fidia kwa wakulima. Hadi Sheria Mpya ya Ardhi ilipopitishwa mwaka 1999, njia iliyotumiwa kulipa fidia ilikuwa imekitwa kwenye Sheria ya Kumiliki Ardhi ya mwaka 1967, kukiwa na marekebisho madogomadogo ya kila mara ya taratibu za ukadiriaji thamani ya mazao; marekebisho ya karibuni kabisa yakiwa yamefanywa mnamo mwaka 1997/98. Mahesabu ya kawaida yalitumika kukadiria upotevu wa mazao, na kwa mazao yaliyokuwa yanazunguka eneo lililohusika kulikuwa na nyongeza kidogo juu ya mapendekezo ya 1998 ili kutatua suala la mpaka. Hata hivyo, Sheria Mpya ya Ardhi, Sheria ya Ardhi ya Vijiji na Kanuni za Ardhi, zinatoa utaratibu mpya wa kufanya tathmini ya upotevu wa ardhi, ambao ni changamani zaidi. Kutokana nahali hiyo, tarehe 15 Oktoba mradi ulishauriwa rasmi na Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi, kwamba "utaratibu wa kufuata mapato ya mwaka kwa zao" kama inavyoelekezwa katika sheria mpya ilibidi ndio utumike kwa Derema badala ya ule utaratibu wa zamani. Kisha utaratibu huo mpya ulitumiwa, na hadi kufikia 7 Novemba njia hii mpya ilionyesha kwamba badala ya kulipa Sh.Tz. milioni 9.31, ambazo ndizo gharama za ulipaji fidia zilizotegemewa, kwa ajili ya ufyekaji wa mpaka, kwa kutumia njia ya zamani jumla ya

fedha hizo sasa ilikuwa Sh. Tz milioni 138 (baadaye zilirekebishwa na kuwa Sh.Tz milioni 138.77 kutokana na ongezeko la mara 12). Matumizi ya sheria mpya hayakuwa yametegemewa, na ni dhahiri kwamba njia hii mpya ilileta mchanganyiko wa mambo na kuchelewesha mchakato: mbaya zaidi, tofauti kubwa kati ya thamani ya zamani na thamani mpya ambayo ililetwa na sheria mpya iliwashtua watu wote waliohusika, na mazungumzo ya kuweka kiwango maalumu kiutawala (Wizara ya Ardhi ilikuwa imependekeza jumla isiyozidi Sh.Tz. milioni 50 mnamo mwezi Novemba, 2001) yakashindikana kutokana na uamuzi wa EUCAMP kufuata utaratibu wa sheria mpya. Ni mwishoni mwa mwezi Machi, 2002, ambapo hatimaye malipo yalifanywa kwa wakulima 172 wa mazao yaliyokuwa katika maeneo ya mpaka, kutokana na bajeti ya EUCAMP.

**13**. Hata hivyo, washauri wa EUCAMP hawakuwa wameelewa vizuri matokeo ya hesabu hizo. Kwa kutegemea tathmini ya mazao ya kwenye “ushoroba” (yale yaliyo katika mipaka) walikadiria kwamba iwapo wakulima 127 walipata Sh.Tz. milioni 113 kwa uwekaji mipaka basi kufidia wakulima 1090 katika mipaka iliyokuwepo kwa pato hilohilo la mwaka zingehitajika Sh.Tz. milioni 800. Hesabu hii, ambayo haikuwa rasmi, haikuzingatia kwamba tafauti katika eneo lililolimwa mazao pia ingekuwa kubwa sana; ukweli ukawa kwamba tafauti ilikuwa hekta 8.1 katika maeneo ya mipaka na kufikia hekta 956 katika mashamba ya ndani ya mipaka. Siyo kwamba mashamba yote yalikuwa na mazao, lakini maeneo yaliyolimwa yalikuwa makubwa zaidi kuliko ule ushoroba wa mita tatu.

**14**. Katika kila eneo husika wakulima mara moja wakajifunza jambo moja muhimu na la wazi zaidi, na bado wanaliongelea. Katika tathmini kamili ya mazao ya mipaka, kwa kutumia sheria mpya, kila mmea wa iliki ulipewa thamani ya Sh.Tz. 28,800, kwa msingi kwamba hiyo ndiyo thamani ya miaka mitatu ya upotevu wa uzalishaji wa zao hilo toka lilipokatwa hadi hapo mazao mapya yangelilimwa katika mashamba mapya na kukomaa. Hii ina maana ya mapato makubwa sana kwa wakulima wa ushoroba, na baadhi yao (ambao idadi na shughuli walizofanya si rahisi kuzihakiki kwa sasa) wakaanza mara moja kupandikiza iliki mpya na mazao mengine kabla kazi ya kufanya

tathmini ya mashamba ya ndani ya ushoroba haijafanywa. Hatua sasa ilikuwa imefikiwa ya kufanya tathmini ya mazao ndani ya mipaka ya ushoroba.

**15**. Angalau mbinu za kuorodhesha na kutathmini mazao katika ushoroba zilikuwa wazi. Iliamuliwa kuwa sheria mpya ndiyo itumike; kampuni ileile ya wataalamu wa tathmini ambayo ilifanya tathmini ya mipaka ndiyo ilichaguliwa kufanya kazi hiyo baada ya ushindani wa zabuni kuanguakia upande wao tena. Kuhesabu mazao kulipangwa kufanyika mnamo mwezi Mei na Juni 2002 na kwamba ripoti ya tathmini kamili ilitakiwa iwe tayari mwishoni mwa mwezi Juni. Kazi ya uwandani ilifanywa kikamilifu na kisha matukio haya muhimu yalifuata:

- Ripoti ya rasimu ya tatu na "ya mwisho" juu ya "mazao ya ushoroba" iliwasilishwa na wataalamu wa ushauri 8 Agosti, 2002 ikiwa inaonyesha jumla ya pesa za malipo ya fidia ya Sh.Tz. bilioni 3.261
- Iliamuliwa kuwa pawepo na timu huru ya wanasheria, kutoka Wizara ya Ardhi , ambayo ndiyo ilipaswa kuipitisha hiyo ripoti ya wataalamu wa tathmini, na kutoka katika Muungano wa Kimataifa wa Hifadhi ya Mazingira (International Union for the Conservation of Nature (IUCN) ) Timu hiyo ya wajumbe wawili ilifanya kazi yake katika nusu ya kwanza ya mwezi Februari 2003. Mjumbe kutoka Wizarani alikuwa Mshauri wa Kisheria wa Wizara, na ndiye aliyepaswa pia kuikubali au kuikataa kazi hiyo. Kwamba ilikuwa sahihi kumwita mjumbe wa Wizara "mkaguzi huru" ni suala la mjadala, kwani malipo ya mwisho ya fidia, kwa maoni ya wataalamu wa tathmini hutuoa picha ya welewa wa nini serikali ilifanya katika kuanzisha mbinu mpya za tathmini, hasa kwa kuwa hii ilikuwa ni mara ya kwanza kwa mbinu hizo kujaribiwa. Kwa hiyo mshauri atakuwa mtetezi wa pendekezo la mwisho, kama "mhakiki" na mmoja wa majaji katika wadhifa wake wa kiwizara.
- Kwa vyovyote, timu ilisifia kazi ya uwandani ya wataalamu wa tathmini katika kuhesabu mazao, wakagundua makosa madogomadogo mengi katika uchanganuzi wao wa matokeo, na walipata wasiwasi zaidi kwa kutokuwepo na sababu za msingi za makadirio, ya wataalamu watathmini, ya mapato ya kila mmea, kiwango halisi kilichopelekwa sokoni na bei zilizopatikana

- Timu haikupendekeza mapato mbadala au bei, wakingojea maelezo zaidi kutoka kwa watathmini. Hata hivyo timu ilieleza katika ripoti yake na kwa watathmini kwamba "Timu ya Wakaguzi Huru" ilikuwa inategemea kwamba tathmini ya jumla ya mazao hatimaye itashuka na kuwa takribani theluthi moja ya kiwango kilichopo", au katika sehemu nyingine ya ripoti yake kwamba ""Timu ya Wakaguzi Huru inatarajia kwamba jumla ya pesa itapungua (kufikia kiasi kama 30% ya kiasi cha sasa. Hili litakuwa jambo muhimu la kuzingatia siyo tu kwa kuamulia kiasi na aina ya fidia, lakini zaidi ya yote katika kuamua kama mchakato huu unaweza kuendelea au la." Hakuna chanzo chochote kilichoonyeshwa katika ripoti kuhusu mattarajio hayo, lakini kwa hakika matarajio hayo hayakutokana na uchunguzi mpya, uchangunuzi mwingine wa data kuhusu idadi ya mimea, mavuno, mazao yaliyouzwa, pendekezo la mbinu mbadala ya kutathmini, au welewa mwingine wa nini sheria zinasema. Hata pendekezo kwamba mchakato ungeweza kusimamishwa iwapo tathmini ya chini zaidi ingependekezwa halikuwa limeangalia mambo kwa yakini. Timu ya Ukaguzi ilijua fika, kutokana na utafiti wake wa uwandani kwamba wakulima waliacha kulima mimea yao au kuvuna viungo na matunda yao mara mazao yao yalipohesabiwa, miezi tisa kabla ya kazi yao. Inaelekea kwamba mnamo mwezo Novemba 2001, wakati "makubaliano" ya Sh.T milioni 50 yalipopendekezwa na mshauri wa Wizara, Timu ya Wakaguzi ilikuwa pia imependekeza "makubaliano" ya kiuanasheria kuhusu suala hili na si kwa kufanya tathmini mpya.
- Shirika la tathmini halikuichukulia kwa dhati ripoti ya Timu ya Wakaguzi, isipokuwa katika kipengele kimoja muhimu. Lilileta rasmi nyingine tu ya tathmini, bila masahihisho ya ziada au sababu za kutumia mbinu zao za uchanganuzi. Halikubadilisha tarehe mweshoni mwa muda wake, Julai 31, 2002. Lakini kwenye ukurasa huohuo wenye tarehe ya zamani ikatoa jumla tafauti ya malipo ya fidia, kijiji kwa kijiji. Jumla kubwa ikawa Sh.Tz bilioni 1.61, pungufu ya bilioni 2.1 na kufikia 35% ya kiasi cha zamani. Bila maelezo ya ziada Mtathmini Mkuu wa Serikali akaipitisha ripoti hiyo ya ukaguzi tarehe 23 Julai, 2003.
- Wakati huo mradi wa EUCAMP ulikuwa unafikia mwishoni. Baada ya awamu tatu za msaada kutoka Serikali ya Ufini, kuanzia mwaka 1987, mradi ukafikia ukomo mnamo Desemba 2002. Ripoti ya kumalizika kwa mradi iliyotolewa na Meneja wa Programu na Mshauri Mkuu wa Kiufundi inahitima kwamba: "Sheria mpya ya Ardhi

imeathiri kwa kiasi kikubwa zoezi la hifadhi ya Derema. Bei za fidia ya mazao imepanda kwa zaidi ya mara tano, kwa hiyo pesa iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya fidia haikuweza kutosha. Iwapo ulipaji wa fidia utashindikana wenyeji wa eneo hilo watakuwa hawana imani na serikali, na hii inaweza kuathiri shughuli za hifadhi katika Milima ya Usambara, kutokana na mgongano wa maslahi unaoweza kutokea."[3]

- Ripoti ya kukamilisha awamu ilieleza kwamba "kiasi kikubwa cha fedha kinahitajika kwa ajili ya mchakato huo wa ulipaji fidia, kulitangaza rasmi eneo, na baadaye matayarisho ya mipango ya usimamizi halisi. Iwapo hakutapatikana fedha za ziada nje ya mchango wa Serikali ya Tanzania, siyo tu kwamba itashindikana kulitangaza rasmi eneo hilo na kupoteza kitegauchumi bali pia kutakuwa na mgongano baina ya wenyeji wenyewe kwa wenyewe, na watunga sera, na asasi za hifadhi katika mkoa wa Tanga." EUCAMP ilipofunga, pesa kadhaa nusunusu zikapatikana kwa ajili ya malipo yaliyopitishwa na maamuzi ya Mtathmini Mkuu wa Serikali (na utangazaji rasmi, usimamizi na uendeshaji wa wa eneo hilo utakuwa ni lengo linaloungwa mkono na Mfuko wa Hifadhi ya Milima ya Tao la Mashariki ambao unapata msaada kutoka GEF). Mnamo mwaka 2004, Serikali ilitoa Sh. Tz. Milioni 100 kwa ajili ya zoezi la ulipaji fidia, Serikali ya Ufini ikakubali kutoa Euro 160,000, ambazo bado hazijalipwa zikingoja makubaliano ya jumla na Serikali zote mbili yakionyesha msaada wa Ufini. Mnamo mwezi Machi 2005 Conservational International (US) Global Conservational Fund ikatoa msaada wa dola za Kimarekani $ 350,000 kwa ajili ya zoezi hilo. Hatimaye mfuko wa Critical Ecosystem Partnership Fund (WWF) umeahidi kutoa dola za Kimarekeni $150,000 kulipia uwezeshaji wa zoezi la ulipaji fidia, utangazaji rasmi wa ushoroba na uanzishwaji wa Mkataba wa Usimamizi wa Pamoja na jumuia zilizopo katika hatua za mwanzo. Fedha hizi zinakuwa ni kiasi kama $650,000 kwa ajili ya kulipia fidia, ukiongeza za CEPF $150,000. Lakini hadi kufikia Aprili 2005 ni Sh.Tz milioni64.8 tu (karibuUS $ 53,000) ndizo likwishafika katika akaunti ya benki ya Muheza, inayohusika na ulipaji fidia.

- Mnamo mwezi Juni 2004 Wizara ya Maliasili na Utalii ilipeleka maombi kwa

---

[3] Programu ya Usimamizi wa Hifadhi ya Eneo la Usambara Mashariki: Ripoti ya Kukamilisha Awamu III (1999 – 2002), Ripoti ya Utawala 40, Wizara ya Maliasili na Utalii, Tanzania (Idara ya Misitu na Ufugaji Nyuki), na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, Ufini (Indufor/Metsähallitus Group) Tanga, Desemba 2002, uk. 49.

Mameneja wa Benki Wasimamizi (pamoja na GEF)wa mradi wa msitu wakioomba fedha za kuongezea kwenye zile zilizokuwapo ili kuweza kutoa malipo mazuri kwa ulipaji fidia uliokubaliwa 2002. Jibu la msingi la Benki, baada ya majadiliano zaidi, lilikuwa ni kutaka kupewa Mpango wa Utekelezaji wa Uhamishaji watu ambao utakuwa unaendana na Sera ya Uendeshaji (OP 4. 12) ya Benki, na hati hii ya sasa inawasilishwa katika jumla ya kutekeleza masharti hayo.

- Wakati huohuo, kadri vuguvugu la Oktoba 2005, la kugombea urais lilipozidi, mamlaka husika wakaanza kuwa na waiswasi juu ya chuki iliyokuwa ikiongeza katika Wilaya ya Muheza kuhusu ucheleweshaji wa malipo ya fidia (maswali yakaulizwa Bungeni). Hali hiyo ilisababisha hatua mpya ya kuanzisha malipo hayo, na Wizara ya Maliasili na Utalii ikatoa 50% ya kiwangio kilichokuwa kinadaiwa (kiasi kama milioni 600). Baada ya kuhakiki ratiba za malipo kijiji baada ya kijiji 50% ya malipo yaliyokuwa yameamuliwa katika mchakato wa 2002/2003 yalilipwa kwa kila mwanakijiji aliyeathirika, kati ya Oktoba 3 -10, 2005. (Uchaguzi ilikuwa ufanyike Oktoba 30, lakini uliahirishwa hadi Desemba 14). Muda huo ulikuwa ni miaka mitatu na nusu tangu mazao yalipoorodheshwa katika ushoroba huo.

**16** Ama kuhusu ulipaji wa fidia katika Derema, kufikia katikati ya mwaka 2006 kulikuwa na maswali kadhaa yaliyokuwa yanahitaji majibu toshelevu, na Mpango huu wa Uhamishaji ulipewa dhima ya kuyatafakari:

(a) Je, tathmini iliyokubaliwa Tanzania, mnamo mwaka 2003, ilikuwa inakubaliana na sera ya Benki ya Dunia (OP 4.12) inayotumika kuhusu uhamishaji watu? Kama sivyo, ni marekebisho gani kuhusu maamuzi ya 2003 ya ulipaji fidia (na hatua nyingine) yanahitajika kufanywa?

(b) Kutokana na kupita muda mrefu toka mazao yalipohesabiwa na kuorodheshwa, inahitajika tathmini mpya au namna fulani ya malipo ya riba, ambayo ni zaidi ya malipo ya fidia yaliyokubaliwa mwaka 2002 na 2003? Je, mahesabu ya ziada yoyote ya aina hiyo yafanywe vipi?

(c) Je, Benki ya Dunia italikubali wazo la kuhamisha fedha katika Mradi wa Hifadhi na Usimamizi wa Misitu (MHUMT)(Tanzania Forest Conservation and Management Project (TFCMP)). Kutumika katika kulipia fidia ya Ushoroba wa

Derema? Je, Kamati Kuu ya Ardhi ya Benki ya Dunia pia itaridhia uhamishaji huo wa fedha, kulingana na sharti la OP 6.0, Kiambatisho A cha Aprili, 2004?

**Athari za Mradi**

**17** MHUMT, unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, haukuingiza masuala ya vitegauchumi au misaada mingine katika Ushoroba wa Derema; wala haikujishughulisha na hali iliyopo pale.

**18**. Mikakati na kazi ya hifadhi ambayo imekuwa ikiendelea tangu miaka ya mwanzoni mwa 1990 imedhihirisha kwamba jitihada zinapaswa kufanywa kuzuia kuendelea kuharibika kwa misiti ya Usambara mashariki na pale ambapo inawezekana kubadilisha muundo na kufanya msitu mmoja unaoendelea. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tunalinda eneo hili lenye ubioanuwai kwa kuanzisha shoroba au kuongeza hifadhi ya ardhi ya taifa. Kituo cha Hifadhi ya Mazingira cha Amani (HIMAA) ilipoanzishwa mnamo mwaka 1998, kwa kuunganisha hifadhi sita za misitu zilizokuwepo na kipande kirefu cha msitu uliokuwa unamilikiwa na Kampuni ya Chai ya Usambara Mashariki, chini ya makubaliano rasmi ya kulilinda eneo hilo, hatua muhimu iliyokuwa inafuata ilikuwa ni kuweka mipaka, kuulinda na kuutangaza rasmi Ushoroba wa Derema

**19**. Ili kuweza kufanya hivyo mipaka ya Derema ilichorwa kwanza na kisha eneo hilo likapimwa mnamo mwaka 2001. Wakulima katika vijijini jirani walishauriwa juu ya usimamizi wa pamoja kwa njia ya kila kijiji kusimamia kipande fulani cha msitu wa hifadhi; lakini wao walipendelea zaidi mkakati wa kuwepo na Hifadhi ya Msitu ya Taifa, ambapo vijiji vingepewa kusimamia maeneo ya hifadhi hiyo kwa utaratibu wa wao nao kupata marupurupu ya pamoja kwa kuutunza msitu. Utaratibu wa namna hii ulikwishakuwepo huko nyuma. Vijiji 16 katika eneo linalozunguka HIMAA viliunda umoja wa kulinda eneo moja lililozuiliwa kwa makubaliano ya kulipwa sehemu ya mapato ya HIMAA na marupurupu mengine.

**20** Vijiji vitano vilishiriki; vitatu vikiwa upande wa magharibi wa Derema na viwili vikiwa mashariki (taz. Kiambatisho 1 kinachoonyesha ramani ya Derema). Vijiji hivyo ni Kisiwani, Kwemdimu,Msasa IBC (jina linalotokana na Kampuni ya kukata magogo iliyokuwepo katika eneo hilo kuanzia miaka ya 1950 hadi miaka ya 1980), Kwezitu na Kambai. Sio kila mkulima alikuwa akilima Derema. Wakati wengi walikuwa na shamba mojamoja msituni, wachache walikuwa na mashamba mawili au zaidi. Jedwali lifuatalo linaonyesha idadi ya watu, idadi ya wakulima walioathirika, na idadi ya mashamba yaliyoathirika katika kila kijiji.

*Jedwali 1*

*Ushoroba wa Derema: Idadi ya watu katika kila kijiji, wakulima walioathirika na mashamba yaliyochukulia*

| **Kijiji** | **Idadi ya Watu (2006)** | **Wakulima walioathirika** | **Mashamba yaliyochukuliwa** |
|---|---|---|---|
| Kisiwani | 689 | 59 | 74 |
| Kwemdimu | 1617 | 244 | 265 |
| Msasa IBC | 2200 | 570 | 744 |
| Kwezitu | 2311 | 216 | 420 |
| Kambai | 1061 | 39 | 44 |
| **Jumla** | **7878** | **1128** | **1547** |

*Chanzo:Idadi ya watu kutoka kwa makatibu wa vijiji; watu walioathirika na zoezi hilo kutoka Tathmini ya Proper Consult ya 2002*

**21** **Kupunguza Makali ya Athari:** Sera ya Benki ya Dunia, ya Uhamishaji Makazi, ikienda pamoja na utunzaji mzuri wa mazingira inahitajia kwamba athari zenye madhara makubwa ziepukwe au zipunguzwe sana. Kwa upande wa Derema mchanganuo wa kiekolojia ulionyesha kwamba ushoroba huu ulihitaji kutangazwa rasmi kuwa mali ya taifa na kufanywa hifadhi, kwamba ulimaji mashamba katika ushoroba huo ulihitaji kukoma kabisa, na kwamba kwa hapo baadaye iwe ni bidhaa chache kabisa za msituni ambazo zitaruhusiwa kuchukuliwa. Njia mbadala kadhaa zilifikiriwa. Kwanza katika vikao na wanavijiji mnamo mwaka 2001 ilipendekezwa kwamba eneo hilo lisimamiwe kama misitu midogomidogo inayolindwa na vijiji kadhaa, kukiwa na taratibu za ndani ya

kila kijiji za ulimaji. Kwa sababu ambazo hazikuandikwa pendekezo hili lilisemekana kukataliwa na badala yake ikapendekezwa kwamba pawe na ulinzi kamili wa ushoroba huo kama hifadhi ya msitu ya taifa. Pili, hekta 956 za eneo lililopangwa kuchukuliwa kama hifadhi zingeweza kurejeshwa kwa wananchi ili kupunguza idadi ya mashamba ambayo yangeathirika. Tatu, mipaka ya hifadhi ingeweza kuhamishwa kwa namna fulani ili kuchukua mashamba machache zaidi, ili kuacha maeneo ya kilimo cha chai. Hata hivyo, hatimaye hakuna hata moja kati ya mapendekezo haya lililokubaliwa. Kwa vyovyote vile, hapakuhitajika uhamishaji wa makazi wowote kwani mpaka uliwekwa mbali, sehemu ya kaskazini mashariki ili kuacha kijiji cha Kwemdimu kubakia kilipokuwa bila kuleta bughudha kwa makazi au mashamba ya chakula kwenye maeneo ambayo hayakuwa ya msitu.

**Watu Walioathirika**

**22**. **Mitaala ya kijamii-kiuchumi:** Mkazo unaowekwa kwenye ekolojia ya Milima ya Usambara Mashariki umewekwa sambamba na jamii zinazozunguka maeneo hayo. Hasa, shirika la WWF limefadhili tafiti mbili juu ya athari za kijamii zinazotokana na shughuli za hifadhi katika kituocha Hifadhi ya Mazingira cha Amani (HIMAA)) na Ushoroba wa Derema uliopendekezwa kuanzishwa.

**23.** **Utafiti wa kwanza,** uliofahamika kama *Conservation and Poverty: A Case Study of the Amani Nature Researve* (*Hifadhi na Umasikini: Uchunguzi Kifani wa Hifadhi ya Mazingira ya Amani*[4]*)* ulihusu vijiji vitatu katika eneo linalopakana na kituo kipya kilichoanzishwa cha HIMAA. Utafiti ulichunguza athari za kuanzishwa kwa HIMAA, mwaka 1997 na kugundua matatizo mengi ambayo yangejitokeza tena na tena katika kuongezeka kwa eneo la Ushoroba wa Derema. Eneo lililozuiliwa (buffer zone) lilianzishwa kuzunguka HIMAA, ikiwa na maana kwamba mamia kadhaa ya wakulima iliwabidi waache viwanja na mashamba yao, lakini ni kiasi cha asilimia 20 – 25 tu ya fidia iliyopaswa kulipwa ndiyo ililipwa; moja ya sababu ikiwa kwamba baadhi ya mazao yalichukuliwa kuwa hayalipiwi fidia. Aidha, siyo matumizi yote ambayo hayakuwa ya

[4] George Jambiya na Hussein Sosovele, *Conservation and Poverty: A Case Sstudyof the Amani Nature Researve*, Research on Poverty Alleviation (REPOA) rripoti 0.5. 2001, Dar es Slaam.

mbao katika Hifadhi hiyo yaliingizwa katika mikataba ya wanavijiji --- watu walilalamikia masharti ambayo mikataba ya eneo lililozuiliwa iliweka, lakini zaidi hasa juu ya kutokuwepo na taarifa zozote muhimu. Watu waliahidiwa ardhi mpya nje ya Amani, lakini ikaja kudhihirika kwamba ardhi hiyo haikuwa kubwa ya kuweza kuwatosha wakulima wote walioathirika. Zaidi ya nusu ya watu wa eneo hilo waliona kwamba miongoni mwa wadau wa eneo hilo wao waliambulia kidogo sana katika kuanzishwa kwa HIMAA. Waandishi wa utafiti huu wakahitimisha kwamba "mahitaji ya jamii ya eneo hilo na ya Taifa yanagongana na yale ya walinzi ubioanuwa (uk.38). Chuki iliyoripotiwa katika vijiji vya Amani katikati ya miaka ya tisini, ilikwishadhihirika pia katika vijiji vya Derema katika miaka ya 2000.

**24. Utafiti wa Pili:** Utafiti wa pili ulikuwa ni wa athari za kijamii za Ushoroba wa Derema wenyewe, uliofanywa kabla mipaka ya hifadhi haijapimwa au hasara za upotevu wa mazao hazijatathminiwa. Kwa kutumia hojaji maalumu na majadiliano ya kikundi maalumu cha wanavijiji kama 300 na viongozi wa vijiji, utafiti ulifanya mchanganuo wa sifa za kijamii-kiuchumi za watu ambao wangeathirika katika vijiji vitano pembizoni mwa Ushoroba. Utafiti ulijaribu pia kupata uelewa wao kuhusu athari ambazo zingewapata juu ya kilimo chao kwa kuupoteza Ushoroba, na masuala waliyoibua juu ya hifadhi hiyo kutangazwa kuwa mali ya serikali

**25. Watu wa Milimani.** Watu wa milima ya Usambara Mashariki hutoka sehemu mbalimbali. Takribani wote, tukiacha wafanyabiashara wachache, walimu, na wafanyakazi wa ujira, huishi kwa kutegemea kilimo chao au ujira wa kufanya kazi katika mashamba makubwa pamoja na vyakula vyao wenyewe. Ni asilimia takribani 56 tu ya watu waishio katika vile vijiji vitano ndio waliozaliwa maeneo hayo. Theluthi moja ya idadi ya watu wa hapo walitoka katika maeneo mengine ya wilaya, ama kutoka vijiji vingine vya milimani au kutoka kwenye tambarare zinazozunguka milima. Moja ya kumi ya wakazi wa hao hutoka katika wilaya nyingine mkoani Tanga, na asilimia 1 ya mwisho wanatoka sehemu nyingine za Tanzania. Uhamiaji mkubwa katika maeneo haya ulisababishwa na fursa za kazi zilizokuwako huko milimani. Kazi ya ukataji magogo (halali na haramu), iliyofanyika mapema zaidi, na baadaye zaidi mashamba ya chai,

ndivyo vilivyoleta msukumo mkubwa wa uhamiaji huo. Kwa kuwa Kibondei, lugha ya watu wa nyanda za chini, na Kishambaa, lugha ya watu wa milimani, ni lugha zinazoelewana, na kwa kuwa, kwa vyovyote vile kila mmoja wao anazungumza Kiswahili, hakuna hali ya uhasama ya kutisha, au tofauti za kikazi au aina nyingine zilizokuwepo. Waislamu na Wakristo huishi kwa kuchanganyikana, hata katika familia zao. 97% ya wakazi wa hapo ama wana kiasi fulani cha elimu ya msingi au wamemaliza kabisa elimu ya msingi, ingawa kuwepo kwa ngazi hii ya kunazidi kupungua thamani katika Tanzania ya leo.

**26.** Kuna umoja wa hali ya juu katika vitongoji vya vijiji katika hivyo vijiji vitano. Vitongoji hivyo huachana kwa umbali wa mita kadhaa pembizoni mwa njia au barabara chini kabisa ya miteremko ya milima ya misitu. Baadhi ya vitongoji hivyo ni vidogo na hukaliwa na vikundi vya kinasaba ambavyo kila kimoja kiko chini ya mzee wa kiume mmoja. Vitongoji vingine ni vikubwa zaidi ambavyo vimekitwa katika mahusiano ya jamii pana zaidi au katika ujirani wa kijiografia baina ya watu wanaotumia maeneo ya wazi ya kilimo chini ya miteremko ya vilima. Nyumba nyingi zilizoko hapo ni za vyumba kuanzia kimoja hadi vitatu, za mbavu za mbwa na zilizoezekwa kwa nyasi; ni nyumba chache tu zenye kuezekwa kwa bati. Kila kitongoji huchukulia kwamba eneo lao linaanzia kwenye nyumba zao na kurudi nyuma hadi kufikia misituni. Ushoroba wa Derema bado haujatangazwa katika gazeti la serikali, na ndiyo sehemu ya juu ya vijiji hivi.

**27** Ukubwa wa mashamba hutofautiana, kuanzia eka 1 hadi eka 40, ploti zikihesabiwa ndani na nje ya misitu. Wakulima wote, kasoro asilimia 3 tu, wnasema “wanamiliki” mashamba yao, ama kutokana na kuyarithi (kama asilimia 37), kutokana na juhudi zao wenyewe za kuishughulikia ardhi ambayo ilikuwa bado haijamilikiwa (kama asilimia 40), kwa kuyanunua (kama asilimia 20), au kwa kugawiwa wakati wa mpango wa vijiji vya Ujamaa baada ya mwaka 1967. Asilimia 5 wanasema kwamba hupata mapato ya ziada kutokana na kazi za ujira; asilimia 15 wanasema hufanya biashara ndogondogo; na wachache wana maduka au stoo bubu za pombe za kienyeji. Kwa upande wa pesa taslimu wakulima wengi hudai kuwa wana mojawapo ya mazao makuu

ya biashara (iliki, karafuu, pilipili manga na mdalasini), lakini asilimia 20 tu (tarakimu ambayo karibu inaoana na orodha zilizoonyeshwa baadaye katika ushoroba uliowekewa mipaka) ndio walisema hayo yalikuwa ni sehemu ya msitu. Wakulima walidai kwamba walikuwa wanapata mapato makubwa sana kutoka kwa mazao haya. Ingawa kulikuwa na tofauti kubwa baina ya vijiji hivyo vitano, kwa wastani kila mkulima alidai kuwa alikuwa akipata ShT milioni 1.4 kutokana na iliki, ShT 165,000 kutokana na mdalasini, ShT 84,000 kutokana na pilipili manga, na ShT 21,000 kutokana na karafuu. Orodha rasmi ya baadaye inatilia shaka ripoti hizi za binafsi, hasa inapokuwa zilitolewa wakati watu wakijua kwamba kulikuwa na mpango wa mashamba yao kuchukuliwa.

**28.** Wakulima wanajua faida za mazingira na utalii ambazo zingepatikana kutokana na kulindwa kwa ushoroba --- Watanzania walio wengi katika milima wanaelekea kuelewa umuhimu wa ardhi yao kama chanzo cha maji. Hata hivyo, walikuwa sahihi katika kufikiria hasara ambazo wangepata kutokana na kufungwa kwa shughuli za kilimo katika eneo la Derema. Walijua watapata hasara ya kudumu ya mapato yaliyokuwa yanatokana na mazao yao ya biashara katika maeneo ya msitu, mashamba machache ya mazao ya chakula, na ardhi katika msitu ambayo hadi wakati huo ililkuwa mali ya vijiji na familia zake. Walihofia kunyimwa hata mazao ya msituni ambayo si ya mbao, ikiwa ni pamoja na kuni, miti ya kujengea, mboga za majani, vyanzo vya maji, na njia muhimu za msituni ambazo huunganisha vijiji na mashamba. Walijua upotevu wa mapato ulikuwa ni kikwazo upande wa matumizi yao, kulipia matibabu, ada za shule, kodi, na uwezo wao wa kuweka akiba kwa ajili ya mambo makubwa kama kuoa na dharura za kifamilia. Walihofia kwamba kadri usalama wa kijamii ulivyozidi kupungua wasiwasi na kuweza kuathirika haraka vingeongezeka: wanawake na watoto wangeumia zaidi. Kwa upande wao akina mama waliwaomba watafiti wasaidie kuhakikisha kwamba hawatanyimwa kuni na mazao mengine madogo ya msituni mara ushoroba huo utakapotangazwa kuwa mali ya serikali. Ukiacha malipo ya faida na hasara, wakulima wa vijiji ambavyo ilikuwa viathirike baada ya muda si mrefu walichukizwa na kuingiliwa na serikali na kushuka kwa mapato yao ambako kungefuatia.

**29.** Wakifikiria matatizo watakayopata baada ya kupata hasara hizo, wakulima walitaka kujua ni kwa vipi wangeweza kupata ardhi nyingine. Wanajua kwamba baadhi ya vijiji katika milima, na vingi katika tambarare, wana ardhi ambayo haijaendelezwa na ambayo ni zaidi ya mahitaji yao. Baadhi ya ardhi kama hiyo huuzwa kwa bei kubwa sana milimani, na kwa bei rahisi kidogo katika tambarare. Hata Kambai na Kwemdimu, kati ya vijiji vilivyo pambizoni mwa ushoroba, pia vina ardhi. Wanavijiji wengi walitegemea kwamba pesa ya fidia, iwapo ingekuwa ya kutosha, ingetumika kununulia ardhi. Kupata ardhi katika vijiji vingine au kwenye miteremko ya milima katika tambarare za jirani ilikuwa ni dalili ya kulazimika kufanya hivyo; lakini pia ni ishara kwa wanavijiji hawa, wawe wamezaliwa milimani au la, kwamba sasa kuna mzunguko wa kizazi kingine, na kwamba familia mpya zinazoanzishwa, zilizo na maisha bora zaidi, na familia zinazokosa ardhi katika eneo la Derema zitahitaji kutafuta fursa nyingine mbali na "nyumbani" kwao. Wakulima wengi walionyesha kwamba walijua kulikuwa na mashamba ya mkonge yaliyotelekezwa (na mashamba ambayo yalipewa leseni lakini hayakuendelezwa), na kwamba serikali ilikwishajadili uwezekano wa kuyagawa kwa wakulima wa Derema.

**30**. Katika utafiti uliofanywa na Jambiya na Sosovele, wakulima waliulizwa hofu yao kuhusu kufungwa kwa ushoroba kunakotegemewa na fidia inayohusiana nako. Wao walitaka wapewe taarifa zaidi na kuwepo na mchakato shirikishi wa tathmini. Kutokana na yale yaliyotokea baada ya kutangazwa kwa HIMAA kama mali ya serikali, walitaka kuhakikishiwa kwamba ulipaji wa fidia utafanywa kwa wakati na utakuwa wa haki. Wanawake walitaka mamlaka husika zifanye matayarisho makini ili waume zao wasipoteze pesa za fidia inapokuwa fursa za kuzitumia vizuri hazikujitokeza mapema. Kila mmoja alitaka huduma bora zaidi za usafiri na kilimo kuweza kuwaingiza katika awamu nyingine ya maisha yao kwa urahisi zaidi.

**31**. Kwa ufupi, vijiji vitano vya Derema vitakavyoathirika vilifanyiwa uchunguzi ili kuweka msingi na mwongozo kwa wanamipango wa Derema. Watu katika vijiji hivyo, wengi wao wakiwa wakulima wa Kishambaa na Kibondei, walikuwa wanajua vizuri jinsi ambavyo sera na mipango ya kitaifa na ya vijijini kwao inaathiri maisha yao kwa kiwango kikubwa. Ardhi ya vijiji vyao, majirani zao na hali za maisha vimeathiriwa sana

na upasuaji mbao, ardhi kugawiwa wakulima wenye mashamba makubwa, sera za vijiji, kujasiria kilimo cha mazao ya viungo na juhudi za hifadhi. Wakulima wa Derema wanajua kilichowatokea watu walioathirika na kuanzishwa kwa HIMAA. Walikuwa na wasiwasi, na wengi hawakupenda kabisa, juu ya athari zilizokuwa zinakuja kutokana na hasara za upotevu wa mazao yao, ambayo ndiyo yawaleteayo sehemu kubwa ya kipato chao. Walitaka kuwa na hakika kwamba kulikuwa na fursa mpya zilizokuwa zimewekwa kwa ajili yao ili waweze kuendelea na maisha vema.

**Kiunzi cha Kisheria**

**32.** **Sheria ya Tanzania**. Mwishoni mwa miaka ya 90, sheria ya ardhi na kanuni zake vilipitiwa na kufanyiwa marekebisho makubwa. Kwa miongo mingi ardhi ilikuwa imegawanywa katika mafungu mawili makubwa: "Ardhi iliyosajiliwa" iliyokuwa chini sheria ya kisasa (ya wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni); na Ardhi ya Vijiji iliyokuwa chini ya sheria ya kimila. Kuanzia urais wa Nyerere, Siasa ya Ujamaa, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1967, iliipa serikali mamlaka kadhaa yaliyoiruhusu kuchukua raislimali kwa manufaa ya umma, kugawa ardhi ambayo ilikuwa haina mwenyewe na kuweka utaratibu mpya wa matumizi ya ardhi kwa madhumuni ya maendeleo. Mwanzoni mwa karne ya 21 sera mpya za uchumi wa soko zilizokuja katika Tanzania baada ya Nyerere zilihitajia Sheria ya Ardhi kupitiwa upya. Sheria mbili zikapitishwa: Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999, yenye kuhusu ardhi iliyosajiliwa, na ambayo kanuni zake zilipitishwa miaka miwili iliyofuata; na Sheria ya Ardhi ya Vijiji (Na 5 ya mwaka 1999), na ambayo Kanuni za Ardhi ya Vijiji (zinazoendana nayo) zilipitishwa zilipishwa mnamo mwaka 2001, na kuchapishwa katika Tangazo la Serikali Na. 86 la tarehe 4.5.2001. Sheria Mpya ya Misitu ilitangazwa rasmi mwaka 2002; Sheria hii haipingani na sheria hizo nyingine mbili za mwaka 1999 kwa upande wa kanuni za ardhi au kuchukuliwa kama mali ya umma.

**33** Ushoroba wa Derema ni ardhi ya vijiji na iko chini ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji na Kanuni zake. Kanuni 9, 10, na 13-18 zinaelezea misingi na taratibu za kufuatwa katika kufidia ardhi (na mali nyingine) inayochukuliwa kwa manufaa ya umma. Sheria inaagiza malipo ya fidia yafanywe katika upotevu wa riba, au thamani katika mali inayoendelezwa

na hasara katika shughuli nyingine zote za biashara, ikiwa ni pamoja na mazao. Pale ambapo yatahitajika malipo ya usumbufu, usafiri na malazi vifanywe. Ama kwa upande wa ardhi ambayo haina mmiliki malipo ya namna hiyo hayafanywi. Pale inapokuwa hapana budi, na inapasa kuwa, Upotevu wa faida (Kanuni 15) utaainishwa kwa kutumia mahesabu yaliyokaguliwa, na itachukuliwa kwa msingi wa faida halisi kwa mwezi wa shughuli inayoendeshwa kwenye ardhi inayohusika. Mazao ya wakulima wadogo nayo yatatathminiwa kwa namna hiyohiyo, ili kupata mtiririko wa mapato yanayopotea toka kipindi hicho hadi mazao mapya yanapokomaa na kufikia kiwango cha kuleta mapato mbadala ya zao lililopotea. Utaratibu huu unaachana sana na mfumo wa zamani uliokuwa ukifanya kazi chini ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1967 ambapo kulikuwa na lazima ya kuwa na ratiba ya kufanya tathmini ya mazao kila baada ya kipindi fulani kwa msingi kwamba bei za mazao hazikuwa imara sana. Ni tofauti hii, ambayo ilifafanuliwa upya wakati ulipaji fidia wa Derema ulipokuwa unajadiliwa, na ambao ulileta thamani kubwa zaidi kuliko mbinu zile za zamani, ambazo zilionekana kudhoofisha jitihada za kumaliza zoezi la kulipa fidia za Derema. Tarehe 15 Oktoba, Wizara ya Ardhi ilipoufahamisha mradi wa EUCAMP, kwamba sasa itatumia Sheria na Kanuni mpya, mradi uliamini kwamba sheria hiyo mpya ingezingatia ulipaji malipo kamili na yenye kuridhisha, tofauti na ratiba za zamani.

**34. Mbinu za Tathmini.** Njia za kukokotoa “faida iliyopotea” haikuelezwa katika kanuni, lakini imeachwa mikononi mwa watathmini wa umma na wa binafsi, mradi tu zithibitishwe na Mtathmini Mkuu wa Serikali. Ama kuhusu mali nyingine, mazao yanaweza kutathminiwa kwa kutumia mbinu za mapato na uzalishaji. Katika Tanzania hii si kazi rahisi, kwani uzalishaji na masoko ya vijijini haviangaliwi kwa makini, wala hakuna mahesabu yanayokaguliwa ya mashamba ya wakulima wadogo. Wala hakuna ratiba zilizokubaliwa za mazao ya kila mmea kwa mujibu wa hali ya mazingira ya kijiji. Ili kukokotoa faida za matunda, na hasa kwa yale mazao ya viungo, ilikuwa ni lazima kujua wakulima waliuza kiasi gani kwa mtu wa kati katika biashara ya nje, na kujua kiasi hicho kwa kuangalia wastani wa kiasi cha zao lililouzwa kwa mmea. Wastani wa bei ya mazao haya kwa kilo hutunzwa katika ofisi ya Afisa Mazao wa Wilaya, lakini orodha hiyo haitoi taarifa yoyote kuhusu zao mojamoja au wakulima wenyewe. Wakulima

hawaweki rekodi ya mauzo wala gharama za pembejeo zao (ambazo sehemu yake kubwa ni nguvukazi ya watu wa familia zao). Sheria nyingine zinaruhusu mabaraza ya vijiji kukusanya kodi za mazao ya wakulima katika vijiji vyao, lakini jambo hili limekuwa gumu kutekeleza.

**35.** Badala ya kutumia taarifa za mauzo ya moja kwa moja na pembejeo, faida zinaweza kuhesabiwa kwa kutumia msingi wa wastani wa mavuno ya zao kwa kila kizio, wastani wa gharama za pembejeo, na kujua wastani wa hasara inayopatikana kwa zao kabla ya kuingizwa katika soko. Uzalishaji wa vijijini hutofautiana sana kulingana na hali zilizoko katika maeneo hayo mbalimbali, na suala la Derema linakuwa ni la kwanza ambapo malipo yake ya fidia yanafanywa kwa misingi ya Sheria Mpya za Ardhi. Kutokana na hali hiyo wataalamu wa tathmini (waliochaguliwa katika hali ya ushindani) walionelea bora kuhesabu mazao na kuyapa baadhi yake viwango vya uzalishaji wake, toka yale ambayo ndio mwanzo yalikuwa yamepandwa hadi kufikia yale ambayo yanaanza kuzeeka; toka yale yaliyokuwa yametunzwa vizuri hadi yale ambayo hayakuwa yametunzwa vizuri sana. Kwa hiyo, kwa mazao yaliyohesabiwa, na kutathminiwa na yale yaliyokuwa yamekomaa na kutunzwa, yalipewa thamani pungufu katika tija na matumizi ya pembejeo. Tija ya mazao yaliyokomaa inaweza kufanyiwa mahesabu kutokana na kuwaulizia wazalishaji na wanunuzi wa vijijini, lakini siyo kwa kutumia tofauti kati ya uzalishaji na viwango halisi vilivyouzwa. Hata hivyo, kwa upande wa mazao ya viungo ni kiasi kidogo sana cha zao lililozalishwa hupotea katika msururu wa uuzaji, kwa sababu mazao yote manne – iliki, karafuu, mdalasini na pilipili manga – hukaushwa juani tu na kuuzwa kwa wachuuzi; hasa wanunuzi wanaoishi vijijini au ambao wanakuja vijijini kununua.

**36**. Kwa upande wa Derema, mradi wa EUCAMP, chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, ndio ulioanzisha shughuli hiyo. Iliweka mkataba na wataalamu wa tathmini. Ilipotokea kwamba thamani zilizoonyeshwa zilikuwa kubwa sana kuliko ilivyotarajiwa mradi uliajiri “timu huru ya wakadiriaji thamani” kupitia tathmini hiyo na kutoa ushauri.

Timu hiyo iliwasilisha ripoti yake ya mwisho[5] ya tathmini hiyo kwa Mthamini Mkuu wa Serikali (taz. aya 15 hapo juu). Baadaye wafanyakazi wa EUCAMP na washauri walipeleka maombi kwa wafadhili wengine ili kuchangia malipo ya fidia yaliyopitishwa, ikiwa ni pamoja na kupeleka maombi kwa mradi wa misitu unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, ambao nao unasaidia Idara ya Misitu na Ufugaji Nyuki, katika Wizara ya Maliasili na Misitu[6]

**37. Sera ya Benki ya Dunia ya mapato na kulinganishwa na sheria ya Tanzania.** Sera ya Uendeshaji 4.12 (OP. 4, 12) ya Benki ya Dunia kuhusu makazi mapya yasiyokusudiwa inaelezea takribani kanuni zilezile za uhamishaji watu katika maeneo yenye mali za uchumi ambazo zimo katika Sheria na Kanuni za Tanzania . Hizo ni pamoja na:

- Sharti la msingi la kulipa fidia kamili, ya haki na isiyocheleweshwa
- Kujumuisha gharama mbalimbali wakati wa kufanya mahesabu ya fidia, zikiwa zinalipwa kama masurufu ya gharama zisizo za moja kwa moja zinazohusiana na ubadilishaji wa mali (usumbufu, usafiri, n.k.)
- Sharti kawmba fidia ya mazao ihesabiwe kama gharama ya jumla ya uzalishaji uliopotea katika kipindi ambacho shughuli mbadala zinatafutwa ili kurejesha mapato ya mhusika katika hali yake.

**38.** Sheria ya Tanzania inakuwa pungufu kidogo katika kushughulikia mambo ya uhamishwaji kuliko Sera ya Uendeshaji ya Benki ya Dunia katika namna ifuatayo:

- Sera ya Uendeshaji ya Benki ya Dunia (OP 4.12) inahitajia kwamba mambo yote yanayohusu mapato, ikiwa ni pamoja na mpango wa utekelezaji wa malipo ya fidia na ubadili wa mali, yapangwe mapema, na yawe wazi kwa wale wote wanaohusika.

---

[5] "Ripoti juu ya Kuhesabu Mazao na Tathmini ya Mazao yaliyomo shambani katika Eneo lililotengwa kwa ajili ya Hifadhi ya Msitu wa Derema", imetayarishwa na Proper Consult (T) Limited, Dar es Salaam, 31 Julai 2002.

[6] EUCAMP ulikuwa mradi uliokuwa unaisaidia ofisi ya *Tanga Catchment Forest Office (TCFO)*, ya Idara ya Misitu na Ufugaji Nyuki. TFCO inayo mamlaka ya kudhibiti *Catchment Forest Reserves* katika Milima ya Usambara Mashariki (ambayo iko katika Wilaya mbili za Mkoa wa Tanga). Ndiyo iliyoanzisha na kupanga upya hifadhi kadhaa za misitu, ikiwa ni pamoja na HIMAA. Hata hivyo HIMAA inawajibika moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa FBD, siyo kwa TFCO

- Inahitajia kwamba mali zilipiwe fidia kwa thamani kamili na halisi
- Inahitajia kwamba watu wanaopoteza mali zao wapewe fursa ya kuboresha hali zao za maisha, na uwezo wa kupata uzalishaji mali mbadala au namna nyingineyo
- Inahitajia kwamba upangaji wa utekelezaji wa shughuli uwe shirikishi, kwa namna ambayo wale watakaoathirika waelewe kikamilifu ni hatua gani zitachukuliwa katika mchakato wa ulipaji fidia
- Inahitajia kwamba kuwe na mbinu na namna rahisi ambazo zinafanya kazi vizuri katika kutatua migogoro na malalamiko.

**39.** Haitegemewi kwamba kutakuwa na hatua zitakazochukuliwa, kwa upande wa mradi huu, kuibadili sheria ya Tanzania na kanuni zake ili ilingane na mahitajio na masharti ya **OP 4.12**. Badala yake Wizara ya Maliasili na Utalii katika kutafuta msaada wa kifedha kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kutatulia suala hili inakubali kutekeleza Mpango wa Kuhamisha Shughuli za Kipato (MKUSHUKI) kwa mujibu wa Sera ya Uendeshaji ya Benki ya Dunia. Katika kipengele chochote cha mchakato huo ambapo masharti ya Tanzania na Benki ya Dunia yanatofautiana au kusigana Wizara inakubali kufuata zile taratibu ambazo ni muafaka kwa pande hizo mbili na taratibu zake. Pale ambapo sera ya Benki haisemi chochote kuhusu kipengele fulani, Wizara haitatafuta kipingamizi kutoka Benki ya Dunia kutekeleza mpango huu wa MKUSHUKI kwa mujibu wa taratibu na kanuni za Tanzania.

**40**. **Kuliingiza Tao la Mashariki Katika sera ya Benki ya Dunia.** Mradi wa Hifadhi na Usimamizi wa Misitu Tanzania (*Tanzania Forest Conservation and Management Project*), ambao unafadhiliwa na IDA una sehemu kuu mbili na muhimu: msaada wa FBD katika uwezo wa kusimamia na kulinda ubioanuwai wa taifa, ikiwa ni pamoja na hifadhi ya misitu; na kusaidia shughuli za hifadhi katika milima ya Tao la Mashariki. Wakati mradi huo ulipowasilishwa kuidhinishwa na Benki ya Dunia, ilielezwa kwamba:

> "Serikali imekubali kwamba iwapo itatokea, kwa bahati mbaya, kwamba katika utekelezaji wa mradi kutakuwa na lazima ya watu kuhamishwa bila hiari yao, mpango makini wa uhamishaji utatayarishwa na kupelekwa IDA ili upitiwe vizuri kabla hatua zozote za uhamishaji hazijachukuliwa".

Ombi hili la kupitishwa kwa MKUSHUKI kusaidia kutangazwa kwa Derema katika Gazeti la serikali na ulipaji fidia ndivyo vinasababisha dharura hii. Katika kuomba msaada kwa ajili ya programu za vitegauchumi katika Tao la Mashariki, Wizara ya Maliasili na Utalii pia inaahidi kuwasilisha mipango ya MKUSHUKI kwa ajili ya uahamishaji zaidi na ulipaji fidia katika sehemu yoyote katika programu ya Tao la Mashariki, kwa kufuata sharti la OP 4.12 lisemalo kwamba "Sera hii itahusu sehemu zote za mradi ambazo zinatokana na uhamishaji pasi na matakwa ya watu, bila kujali vyanzo vya upatikanaji wa fedha" (**OP 4.12 aya ya 4**). Hili ni sharti muhimu katika kuhakikisha kwamba usimamizi katika Tao la Mashariki, kadri unavyozidi kuongeza shoroba na hifadhi ili kupata maeneo makubwa zaidi ya misitu, hauleti tena uhamishwaji wa wakulima kwa namna zilezile zisizo na uhakika ambazo zimetokea kwa upande wa Derema.

**41**. Makala kutoka mradi wa GEF-UNDP yanabainisha maeneo, katika Tao la Mashariki, ambayo yanahitaji kulindwa[7]. Makala yanabainisha maeneo 11 ambayo "yanahitaji" kutangazwa katika gazeti la serikali na, ambayo yatafanya eneo lote la hifadhi kuongezeka na kuwa zaidi ya hekta 76,000. Maeneo hayo ni pamoja na misitu katika Wilaya ya Mwanga (Kamwala I na II, Kiverenge, Mwala, Kamwenda); Wilaya ya Muheza (ukiacha Derema, kuna Bamaba/Kwamgumi/Segoma, Kwamtili); Wilaya ya Kilosa (Mamiwa-Kisara Kaskazini na Kusini); Wilaya ya Mpwapwa (Kiboriani); Wila ya Kilolo (Kitonga, Kimala); na eneo kwenye Milima ya Rubeho. Pili, makala yanabainisha shoroba zinastahili kuunganishwa, ambazo ni muhimu katika kupunguza mmegeko mkali wa maeneo ya misitu mbalimbali: Maeneo hayo ni pamoja na uwazi wa Bunduki kati ya Uluguru Kaskazini na Kusini, na uwazi wa genge la Matundu-Udzungwa katika milima ya Udzungwa. Tatu, makala yanapendekeza kupandishwa hadhi hifadhi kadhaa kuwa Hifadhi za Mazingira au Bustani za Taifa, hatua ambayo itayafanya matumizi ya maeneo hayo na binadamu kutoruhusiwa kisheria.

[7] Neil Burgess na Felician Kilahama: Ni kiasi gani cha Milima ya Tao la Mashariki kimelindwa na nini kinahitajika ili kukamilisha Mtandao wa Eneo Lililolindwa? Hifadhi na Usimamizi wa Mradi wa Misitu ya Mlima ya Tao la Mashariki. Ripoti Na 2004/3 uk. 3

**42.** Maeneo haya yanabainishwa hapa kwa madhumuni ya kuonyesha tu kwamba yanaweza kuwa maeneo ambayo yanatumiwa sana na watu, na ambayo watu wa maeneo hayo wanaweza kudai kuwa ni maeneo yao. Wazo la kuyahifadhi au kuyapandisha hadhi linaweza kuwa muhimu na la lazima, lakini hatua hiyo haiwezi kuchukuliwa bila ya kufanya uchanganuzi makini wa suala zima, ikiwa ni pamoja na uchanganuzi wa kina na wa kitaalamu wa gharama za binadamu zitakazotokana na kuchukua hatua hiyo. Aidha kutatakiwa pia maelezo kamaili yanayohusu gharama zitakazotakikana katika mchakato wa kutangazwa kwake. Katika muktadha wa MKUSHUKI, na ili kulinda uhai wa mradi, ni muhimu kuhakikisha kwamba kuna uthabiti wa utekelezaji mambo, kusiwe na ugeuheu.

**Kuhamishwa katika Ushoroba**

**43.** **Wajibu wa Kiasasi Tanzania**. Katika Tanzania hakuna wakala mkuu mwenye dhima ya usimamizi wa shughuli zote za ugawaji ardhi kwa makazi mapya. Sheria ya Ardhi ya 1999, Sheria ya Ardhi ya Kijiji ya 2000, na sheria nyingine ndogo za kisekta zinaeleza taratibu zitakazotumika katika ugawaji ardhi na usuluhishaji wa migogoro ya ardhi, lakini usimamizi wa sheria hizo umeachwa katika mamlaka ya serikali za mitaa, serikali kuu na mahakama. Wakala Mkuu atakayeshughulika na usimamizi wa utekelezaji wa Mpango wa Kuhamisha Shughuli za Kipato (MKUSHUKI) ni Idara ya Misitu na Ufugaji Nyuki ya Wizara ya Tanzania ya Maliasili na Utalii (WMU). Tazama sehemu ifuatayo hapa chini kuhusu muundo wa majukumu mbalimbali ya asasi zinazohusika na utekelezi wa Mpango wa Kuhamisha Shughuli za Kipato (MKUSHUKI).

**44** **Kustahiki kulipwa fidia**. Kustahiki kulipwa fidia kwa ajili ya mashamba yaliyochukuliwa katika Ushoroba wa Derema ni jambo rahisi tu. Wale wote waliokuwa na mashamba wanastahiki kulipwa. Mikutano iliyofanyika miaka kadhaa ikiendeshwa na Hifadhi ya Mazingira ya Amani (HIMAA), Wilaya, na washauri wengine wa mambo ya hifadhi walikwishawatayarisha wanavijiji kwa ajili ya malipo hayo. Mnamo miezi ya Mei na Juni, mwaka 2002, timu iliyokuwa ikiongozwa na wataalamu wa tathmini, wakishirikiana na maafisa wa Wilaya ya Muheza, wa mazao, ardhi na kilimo, maafisa wa misitu, na maafisa uwandani wasaidizi wanne , kutoka vijiji vilivyoathirika walipita kila

kijiji. Wanavijiji waliitwa kwenye mashamba yao, na viongozi wa wakulima na wa vijiji wakahakiki mipaka na umiliki wa kila shamba. Kila zao lilihesabiwa mmea kwa mmea, na jani lilikatwa au lilipindishwa kuonyesha kwamba mmea huo umekwishahesabiwa. Kila shamba lilipewa alama yake ya utambulisho na kila mkulima alipigwa picha shambani kwake mbele ya mti ambao una alama ya utambulisho wa shamba hilo. Mimea ilikaguliwa wakati huohuo ili kutambua ukomavu na hali ya kutunzwa kwake. Mahesabu yote hayo yaliorodheshwa kwenye fomu za madai na kutiwa sahihi na mkulima mhusika pamoja na Afisa Ardhi wa Wilaya. Wakulima wote waliambiwa kuweka katika kumbu kumbu alama za utambulisho wa mashamba yao na idadi ya mimea iliyohesabiwa, lakini hawakupewa nakala za fomu zao wakati huo. Waliahidiwa kuwa nakala za fomu hizo zingepelekwa kwa wenyeviti wa vijiji; lakini kwa hakika hazikutolewa wala kupelekwa huko. Kwa mujibu wa matarajio ya awali kabisa ya makadirio yaliyofanywa wakati mazao ya "mpaka" yalipohesabiwa na kufyekwa (wakati mpaka wa mita 3 za ushoroba ulipopimwa kukatwa na kulipiwa fidia mwaka uliopita), ilikuwa imekadiriwa kwamba kungekuwa na mashamba 648; lakini kazi ya kuhesabu ilipomalizika idadi halisi ya mashamba yaliyohesabiwa ilikuwa 1547. Hakuna shaka kwamba sehemu ya ongezeko hili kubwa ilitokana na upandaji wa haraka wa mashamba, mara tu ilipotangazwa kuwa mashamba yangehesabiwa kwa ajili ya kulipiwa fidia. Aidha, ni wazi kwamba kulikuwa na ongezeko jingine kubwa katika vijiji vilivyoongezeka baadaye. Hata hivyo, hata hayo makadirio yenyewe ya mashamba yaliyokuwa yamefanywa yalikuwa ya chini; na kwa vyovyote vile, mashamba yakishaanzishwa baadaye huweza kutoa mazao. Kutokana na kutokuwepo kwa picha za mapema za mashamba hayo au njia nyingine ya upimaji mashamba ya kuwezesha kuweka tarehe ya mwisho ya stahiki ya kulipwa fidia, mradi na serikali havikuwa na njia nyingine isipokuwa kuridhia kwamba kila shamba lililohesabiwa linastahiki fidia. Hakuna taarifa zilizokusanywa kuhusu jinsia, umri au sifa nyingine zozote za kijamii za watu wa kulipwa fidia; majina yao tu ndiyo yanaonyesha nani kaathirika. (Kwa kuangalia orodha ya majina yaliyopo tunaweza kusema kwamba pengine asilimia tano au kumi walikuwa wanawake). Baada ya kazi ya kuhesabu kukamilika, afisa misitu mmoja alibaki vijijini kushughulikia matatizo madogomadogo, ikiwa ni pamoja na wale wakulima ambao hawakuwepo siku za kuhesabu mashamba na wenye malalamiko kuhusu umiliki au urithi wa mashamba. Kesi zote hizo hazikuchukua

muda kutatuliwa, pengine kwa sababu mashamba mengi hayakuwa na umiliki wa miaka mingi. Hakukuwa na suala jingine kuhusu kustahiki fidia; mashamba yote yalihesabiwa, na wakulima wakatambuliwa kwa usahihi kabisa.

**45. Tathmini na Ulipaji fidia ya hasara: zoezi la mwaka 2002.** Njia iliyotumika kufanya tathmini imeelezwa hapo juu. Mazao yaliyohusika yalikuwa ni; iliki, pilipili manga, mdalasini, karafuu, miparachichi, migomba, minazi, viazi vikuu, mikahawa, mipera, kweme, mifenesi, milimau, matunda Malaya, miembe, michikichi, michungwa, mipapai, mikarakara, minanasi, na miwa. Palikuwa na jumla ya mazao 21. Yote haya ni mazao ya miti isipokuwa iliki, viazi vikuu, na minanasi, ambayo ni mimea inayootea chinichini, kila mmoja na nafasi kubwa kubwa, hali ambayo hufanya iwe rahisi kuihesabu; pilipili manga, mmea ambao huhesabiwa kama mtambaaji ambao huota kwa kuitambalia miti yenye vivuli, na miwa. Hapajatokea pingamizi lolote kuhusu kuhesabiwa kwa mimea, iwe ni kwa wakulima wenyewe au timu huru iliyoipitia na kuitolea maoni ripoti ya mtathmini.

**46**. Kila mmea ulihesabiwa kulingana na kiwango cha kuzaa, kuanzia ile ambayo ndiyo mwanzo ilikuwa imepandwa hadi ile iliyokuwa imekomaa na kuanza kuzeeka, ubora wa mmea wenyewe, kuanzia ile iliyokuwa imetunzwa vizuri hadi ile ambayo haikuwa imetunzwa vizuri kabisa. Kwa mfano, iliki, zao lililo muhimu kuzidi mengine yote, limegawanywa katika viwango vitatu vya kukua kwake, kuanzia upandaji mpya (ujulikanao kama “mmea wa siku moja,” ingawa kwa hakika upande wa iliki ni kipandikizi cha kishina-ukoka chenye kikonyo na jani moja), kufikia mmea mchanga uliopandwa miezi kadhaa iliyopita lakini ambao haujatoa mbegu, hadi kufikia mmea uliokomaa. Aidha mimea ya iliki iliyokomaa nayo iligawanywa katika makundi matatu kulingana na ubora wa utunzaji wake, yaani, ambayo imetunzwa vizuri kwa kiasi kikubwa; ambayo imetunzwa vizuri kwa wastani; na ambayo utunzaji wake umekuwa chini ya wastani / karibu imetelekezwa. Katika hiki kiwango cha mwisho, kutambua pia mimea ambayo inazeeka baada ya kuzaa. Ama kuhusu mimea ile ambayo haijachoka pia kulikuwa na makundi mawili, michanga na iliyokomaa. Migomba pia iligawanywa katika makundi mawili ya mimea iliyokomaa, makundi mawili ya mimea ambayo haijakomaa,

na ile iliyopandwa hivi karibuni. Mazao mengi mengine pia yaligawanywa katika kundi moja au mawili ya mimea iliyokomaa, na aghalabu kundi moja la mimea ambayo haijakomaa pamoja na kiasi cha upandaji mpya. Mgawanyo kamili uliotumiwa na watathmini umeonyeshwa katika Kiambatisho 1: Kiambatisho hiki ndicho kile cha awali kilichoatayarishwa na kampuni ya *Proper Consult*, pamoja na marekebisho kidogo (taz. Chini)

**47.** Kwa kila zao, hatua iliyofuata ni kufanya mahesabu ya gharama za uendeshaji. Hizi ni pamoja na gharama za wafanyakazi, kuanzia ufyekaji wa mashamba hadi usafirishaji na ukaushaji, na pembejeo ndogo (hasa miche, kwa sababu hakuna mbolea au viua wadudu vitumikavyo kwa ajili ya mazao katika eneo hili). Makadirio ya matumizi ya nyumbani kwa kila zao lililohusika pia yalifanywa.

**48**. Tukiacha tathmini hii ya mazao yaliyokuwepo shambani, makadirio ya bei za mauzo ya mazao yaliyokomaa yangeweza kufanywa kwa kuwauliza wazalishaji na wanunuzi wa vijijini. Hiyo iliacha pengo kati ya mahesabu ya uzalishaji wa kila kiwango na ubora wa mmea (uzalishaji kwenye "lango la shamba") kwa upande mmoja na kiasi halisi kilichoingizwa katika soko kwa upande mwingine. Hii haikujulikana na ilitofautiana sana kati ya mazao ya viungo, ambayo ni kiasi kidogo tu kinachopotea katika ukaushaji juani, na mlolongo wa masoko (mazao huuzwa zaidi kwa wanunuzi wanaoishi vijijini au wanaotembelea vijiji), na mazao yanayoharibika haraka, kama vile machungwa na mapera. Hata hivyo kwa kutumia uchunguzi mdogo na uchunguzi kadhaa wa uwandani, kampuni ya *Proper Consult* walijitahidi sana kukadiria uzalishaji wa mazao ya biashara kwa kuzingatia ukomavu na ubora wa utunzaji wa mazao.

**49**. Dhana ya ulipaji fidia iliyomo katika Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Tanzania inaelekeza kuwa ulipaji fidia uwe wa kulipa thamani ya upotevu wa uzalishaji wa mazao hadi hapo mazao mapya yatakapokuwa yamepandwa, yakakua na kufikia kiwango cha uzalishaji cha kiasi kama kile kilichopotezwa; ili kuhakikisha kwamba hakuna baki ya hasara ya mapato kwa kipindi chote hicho. Sheria ilichukua "wastani" wa muda wa ukomavu wa zao kuwa miaka mitatu, na hivyo basi mfanya tathmini alifanya mahesabu

ya uzalishaji wa kila mwezi wa kila zao lililokomaa na kuzidisha mara 36 kupata jumla ya thamani ya zao linalohusika. Kwa yale mazao ambayo yalikuwa bado kukomaa yalifanywa makadirio ya uzalishaji wa kila mwaka na kuondoa vipengele ambavyo viliingizwa katika mahesabu ya kipindi cha miezi 36. Hata hivyo mantiki hii haifanyi kazi kwa upande wa Derema. Hasa kwa mazao kama iliki na pilipili manga kwani mashamba ya msituni hayawezi kuwa na mbadala. Hii ni kwa sababu kivuli cha msitu na unyevu wake ni hali zilizo muhimu sana katika uzalishaji wa zao la iliki, zao ambalo linachukua asilimia 74 ya malipo yote ya fidia; pilipili manga pia hustawi vyema katika kivuli. Miti mingine na mazao ya shambani hutofautiana katika kutegemea hali za msitu. Hata hivyo ni kweli pia kwamba katika vijiji vyote kuna vijiji vitatu (Msasa, Kwezitu, na Kisiwani) ambavyo vinaishiwa ardhi kwa ajili ya kupanda mazao zaidi. Miti michache ya viungo au matunda yaweza kupandwa katika vijiji hivi, lakini hakuna kabisa nafasi ya ardhi ya kuanzisha tena mazao yaliyopotea kwa kiwango kilekile yalipopandwa msituni.

**50. Tathmini na Ulipaji fidia ya hasara: masharti ya Benki ya Dunia (OP 4.12) kuhusu hasara ya upotevu wa mazao na miti:** Kanuni ya msingi ya ulipaji fidia, kwa mujibu wa sera ya Benki ya Dunia, ni kwamba watu wanapaswa kulipwa fidia kamili ya thamani ya mali iliyopotea. Sera iko wazi kabisa kuhusu mazao na miti ya biashara: kama ilivyo sera mpya ya Tanzania, sera ya Benki ya Dunia inahitajia kwamba mahesabu yatakayofanywa yazingatie thamani kamili ya mazao yatakayopotea kuanzia wakati huo hadi kipindi kingine ambacho mazao mapya yangepandwa, kukua na kufikia kiwango cha uzalishaji cha hayo yaliyochukuliwa. Ama kuhusu hali ya Derema mambo yafuatayo yanahitaji kuzingatiwa:

- Mazao hayakufyekwa na mamlaka husika baada ya kufanyiwa tathmini. Lakini, watu waliambiwa kwamba wangelipwa fidia ya mazao yao katika kipindi kisichozidi miezi sita; yaani kufikia mwisho wa mwaka 2002. Kama ilivyo kawaida ya watu wote duniani, wakulima wakaacha kuyaendeleza mazao yao, wakavuna kilichokuwepo, na kuyatelekeza mashamba yao. Katika hali na mazingira ya msitu hii ilikuwa na maana kwamba wadudu na wanyama waharibifu walianza kuyashambulia mazao na baada ya miezi kadhaa kupita

msitu ukaanza kuota tena. Watu waliotembelea maeneo yenye mashamba haya wamethibitisha kwamba yametelekezwa.

- Wakulima hawakupata ardhi mbadala au miche ambayo wangeweza kupanda katika maeneo ambayo yangeweza kupatikana, kwa mazao ambayo yangeweza kuota vijijini.
- Kwa hiyo wakulima watakuwa wamepoteza thamani ya mazao yao kwa mwaka 2003, 2004, 2005 na 2006
- Aidha, kwa kutolipwa fidia yao (hadi malipo ya mwishoni mwa mwaka 2005) walipoteza thamani ambayo fedha hizo zingekuwa nayo, kama wangelipwa kwa wakati kabla mazao hayajatelekezwa. Fedha zitakazolipwa sasa zitakuwa zimeathiriwa na mfumuko wa bei; ambapo kama wakulima wangeipata riba hata kama wangeziacha katika benki. Na kwa hakika uwezekano mkubwa ni kwamba wangewekeza katika shughuli ambazo hazina uwezekano mkubwa wa hasara (mazao au mifugo); shughuli ambazo haziathiriwi sana na mfumuko wa bei kuliko kuziweka benki.
- Kama wangelipwa thamani ya uzalishaji wa mashamba yao kila mwaka wangepata malipo ambayo wangeweza kuanza kuyawekeza wakati huo. Hasara ya kila mwaka, kutokana na kutokulipwa kwao kwa wakati imesababisha kupungua thamani kwa fedha yao kuanzia wakati ambapo walipaswa kulipwa.

**51. Mchanganuo wa mahesabu uliorekebishwa kwa kufuata Kanuni za Benki ya Dunia**. Hadidu za Rejea zilizotumika katika ripoti hii zilihitajia uchanganuzi mpya wa malipo ya fidia wanayopaswa kulipwa wakulima. Aidha Benki ya Dunia ilieleza wazi kwamba zoezi hili shurti lifuate viwango vya Benki ya Dunia kama benki itahitajika kuisaidia Serikali katika mpango wa ulipaji fidia uliorekebishwa.

- Kwanza, mahesabu, uanishaji wa viwango vya ubora wa mazao, na tija ya mazao yote (kasoro zao moja tu, taz. maelezo yafuatayo) vilichukuliwa kutoka thamini ya kampuni ya *Proper Consult*. Kwa ujumla maelezo ya “wakadiria thamani” na wanakijiji waliopatikana wakati wa utayarishaji wa MKUSHUKI yanakubaliana kwamba tarakimu hizi ni sahihi.

**RASIMU**

- Kwa mujibu wa hesabu za wakadiria thamani iliki ilichukua asilimia 74 ya mazao yote yalioharibika. Kwa hiyo utafiti wa kazi ya uwandani ulizingatia zaidi thamani ya iliki. Katika utafiti huo uchunguzi ulifanywa kuhusu uzalishaji wa zao hili vijijini, kama zao bichi na kama zao lililokaushwa, kwa kuwatumia wakulima na wafanyabiashara wake, ikiwa ni pamoja na wale ambao waliathirika na matokeo ya uzalishaji wake na wale ambao hawakuathirika nayo. Watafiti uligundua kwamba mchanganuo wa 2002 ulikuwa na makadiria ya juu mno ya uzalishaji wa iliki kwa kila mmea. **Kwa hiyo walirekebisha kiasi cha uzalishaji wa mmea mmoja kwa mwaka kutoka kilo 5 za iliki kavu hadi kilo 3**.
- Kutokana na mabadiliko hayo, mahesabu ya mwanzo ya fidia yaliyofanywa na kampuni ya *Proper Consult* katika miswada yao ya awali, ya ripoti yao (kabla ya mabadiliko yaliyotakiwa baada ya "Ripoti ya Tathmini Huru") yamekubaliwa kwa upande wa uzalishaji (kwa viwango mbalimbali vya kukomaa kwa mimea, wingi na thamani ya soko, kasoro masahihisho madogomadogo ya makosa)). Mafaili, moja kwa kila mkulima, ya mwaka 2002, yaliyotayarishwa na *Proper Consult* yakarekebishwa vilivyo, na yanapatikana katika mafaili ya mradi katika MNRT/FBD, ambayo yatatumika kwa ajili ya malipo.
- Mfumuko wa Bei ya shilingi ya Tanzania, kuanzia mwaka 2003 hadi mwaka 2006, **wakati halisi wa malipo**, kutaongezwa kwenye malipo ili kuondoa hasara waliyopata wakulima kwa kutopata fedha zao mwishoni mwa mwaka 2002. Maelezo ya thamani ya malimbikizo ya mfumuko wa bei yanapatikana katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwezeshaji kama ifuatavyo: **Viwango vya Sasa ni kama vifuatavyo na vitarekebishwa wakati wa zoezi la utekelezaji wa malipo ya fidia ya MKUSHUKI:**

*Jedwali 2*

MUUNDO WA VIWANGO VYA RIBA NA MFUMUKO WA BEI: TANZANIA (KTK %)

| | 2003 | 2004 | 2005 | 2006[2] |
|---|---|---|---|---|
| Benki za Biashara: | | | | |
| Viwango vya Uwekaji Benki- Sarafu ya TZ | | | | |
| Akiba | 2.5 | 2.4 | 2.6 | 2.6 |
| Ya Muda Maalumu (miezi 3-6) | 3.5 | 4.3 | 4.4 | 4.4 |
| Riba ya Mali isiyohamishika[1] | -1.0 | -1.9 | -1.9 | -3.2 |
| Mfumuko wa Bei (wastani wa mwaka) | 3.5 | 4.3 | 4.5 | 5.8 |
| **Limbikizo la Mfumuko wa Bei Januari 2003 – Desemba 2006** | | | | **18.1** |

1/ Imetokana na viwango vya riba ya uwekaji akiba benki vya benki za biashara
2/ Imechukuliwa kwamba tarakimu za Desemba 2005 zimelibakia zilezile mwaka 2006
Chanzo: Ofisi ya Rais – Mipango & Uwezeshaji, Jamhuri ya Muungani wa Tanznia, ***Uchunguzi wa Kiuchumi***

- Tarakimu za thamani ya limbikizo la mfumuko wa bei iliongezwa kwenye malipo yote yaliyotakiwa kulipwa, mwaka 2002 (bila kutoa malipo ya mwishoni mwa mwaka 2005)
- Jedwali lifuatayo linaonyesha matokeo ya kila kijiji, kwa kila zao. Jedwali la mwongozo kwa mazao yote na vijiji ni kama ifuatavyo:

*Jedwali 3*

JUMLA YA FIDIA ILIYOREKEBISHWA AMBAYO INAPASWA KULIPWA KUFIKIA MWISHO WA MWAKA 2006, KWA MAZAO YOTE YALIYOORODHESHWA NA VIJIJI (Sh Tz)

| **KIJIJI** | **MAZAO** | | | | | | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **ILIKI** | **PILIPILI MANGA** | **KARAFUU** | **MDALA-SINI** | **NDIZI** | **MENGI-NE YOTE** | |
| KISIWANI | 4, 610, 910 | 1, 319, 975 | 1, 003,200 | 96, 242 | 3,351,270 | 1,691,963 | 12,073,560 |
| KAMBAI | 6,025,191 | 186 | 685,140 | 2,300 | 200,021 | 435,611 | 7,348,449 |
| KWE-ZITU | 3,56,439,969 | 103, 465 | 6,289,940 | 321,747 | 12,983,802 | 4,944,736 | 381,083659 |
| KWE-MDIMU | 445,802,512 | 1, 572,243 | 1,406,260 | 143,959 | 9,108,422 | 3,084,343 | 461,117,967 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MSASA IBC | 1,230,348,512 | 2,492,447 | 72,571,626 | 3,655,427 | 84,669,044 | 23,709,766 | 1,417,446,822 |
| JUMLA | 2,043,227,322 | 5,488,316 | 81,956,166 | 4,219,675 | 110,312,559 | 33,866,419 | 2,279,070,457 |
| JUMLA NA MFUMUKO WA BEI | | | | | | | 2,730,326,407 |

Chanzo: Hesabu mpya imekitwa kwenye hesabu na mchanganuo wa mazao wa mwaka 2002.

**52** Mfumuko wa bei unaongeza asilimia 19.8 kwa kila mojawapo ya namba hizi, kwa fidia ya kila mkulima, na hivyo basi kwa jumla ya pesa yote itakiwayokulipwa. Jumla ya fidia inayopaswa kulipwa kufikia mwishoni mwa mwaka 2006, ikiwa pamoja na nyongeza ya mfumuko wa bei ni Sh. Tz 2, 730, 326, 407, au dola za Marekani $ 2, 184, 261 kwa kiwango cha Sh Tz. 1250 kwa kila dola. Maelezo zaidi kuhusu jedwali hili yanahitajika. Kiasi kitakikanacho kulipwa, kwa namna fulani, ni pungufu ya mahesabu yaliyokuwa yamefanywa na kampuni ya *Proper Consult* hapo awali, kutokana hasa hasa na kupunguka kwa tija ya iliki kulikotokea wakati wa zoezi la mchanganuo wa sasa. Kulipa nyongeza ya mfumuko wa bei hakuvunji sheria za Tanzania wala kanuni za Benki. Inatoa mwanya wa kulipa fidia ya haki, kitu ambacho ni msingi wa sheria linganishi ya kimataifa karibu kila mahali. Kulipa mfumuko wa bei ni utaratibu wenye manufaa zaidi kuliko kulipa kwa kutumia viwango vya riba za akaunti za akiba za benki za Tanzania, kama ambavyo inaonyeshwa pia katika Jedwali 1; kwani riba za akaunti za akiba haziendi sawa na mfumuko wa bei. Aidha, ni muhimu kukumbuka pia kwamba katika kipindi hiki cha zaidi ya miaka minne ya mazao, tangu mazao yachukuliwe, nguvukazi ya mwanakijiji imekuwa ikitumika kwingineko; kwa hiyo itakuwa ni haki pia kutoa gharama za nguvukazi na pembejeo nyingine katika thamani ya mazao yaliyolimwa, kama ilivyofanywa katika mahesabu.

**53.** **Hatua za kurejesha upatikanaji wa mapato:** Hatua za ulipaji fidia ambazo zitawawezesha wakulima kurejesha namna ya kupata mapato yao zinahitajika. Tukizingatia kwamba katika hivyo vijiji vitano hakuna ardhi, kuna seti mbili kuu za hatua zitakazochukuliwa. Hatua ya kwanza ni ile ambayo inaendelea na kupanuka ya ujasiriamali wa shughuli makini za kilimo ambazo zimeanzishwa katika vijiji

vinavyozunguka kituo cha Hifadhi ya Mazingira cha Amani (HIMAA) (Amani Nature Reserve (ANR)), au katika vijiji vyote vya eneo hilo ikiwa ni sehemu ya miradi ya Mashirika Yasiyo-ya-Kiserikali (NGOs), au kama hatua dhahiri za makusudi za kuboresha mapato katika Kanda iliyozuiliwa ya HIMAA. Hatua ya pili ambayo itaweza kuleta kutengenea kwa mapato ni kuwagawia watu ardhi katika maeneo yaliyokuwa yamelimwa zamani, katika nyanda za chini mashariki ya Derema.

**54.** **HIMAA** ilipoanzishwa mnamo mwaka 1997, uongozi wake ulifikia mapatano na vijiji 18 vinavyozunguka kituo hicho na kulifanya eneo hilo kuwa Kanda iliyozuiliwa na ambalo linaendesha Mpango wa Pamoja wa Utunzaji Misitu unaoendelea. Mpango huu umekitwa kwenye matokeo ya jitihada za IUCN katika miaka ya 1980 za kuanzishwa kwa Maendeleo ya Vijijini yaliyokitwa katika hifadhi[8]. Nia imekuwa ni kupunguza uharibifu wa misitu, kwa kuboresha kilimo katika maeneo jirani. Kutokana na kuanzishwa kwa HIMAA shughuli za uzalishaji mapato, elimu ya mazingira, na hifadhi ya misitu katika vijiji vikafanywa sehemu ya mpango wa kuvisaidia vijiji. Nao wanavijiji katika kuitikia mpango huo wamekubali kupunguza ukusanyaji kuni msituni hadi kufikia mara mbili tu kwa wiki, kuchuma mimea ya dawa kwa ruhusa maalumu tu (juhudi zikiwa zinafanywa kuruhusu waganga wa jadi tu ndio wachume mimea au miti inayohusika), na kuwapa ushirikiano watafiti, mabwana misitu, na wanahifadhi. Motisha zimewekwa wazi: siyo tu kwamba kuna shughuli za uzalishaji mali bali pia hivyo vijiji kumi na vinane hugawana asilimia 20 ya kiingilio na malipo ya utafiti katika HIMAA, na kiasi cha mauzo ya mbao ambazo zimekatwa isivyo halali ambazo zimekamatwa kwa juhudi za wanavijiji. Hivi karibuni ugawanaji huu wa mapato umefikia takribani Sh. Tz. milioni 2.6, au kiasi kama Sh. Tz. 145,000 kwa kila kijiji kwa mwaka. Viongozi wa kijiji cha Derema wanataraji kwamba wataingizwa pia katika mgao huo, Derema itakapochapishwa katika gazeti la Serikali.

**55** Shughuli za uzalishaji mapato zimekuwa anuwai (za aina mbalimbali). Zote zimeelekezwa kwa mwanakijiji binafsi kufanya ubunifu wake kulingana na mwanya

---

[8] Maelezo ya mipango hii yameelezwa katika Heini Vihemäki, “Politics of Participatory Forest Conservation: Cases from the Rast Usambara Mountains, Tanzania,” katika Journal of Transdisciplinary Environmental Studies, Vol. 4, no. 2, 2005, uk. 16. Kwenye Tovuti ni http://www.journal-tes.dk,

unaopatikana, mapendeleo na uwezo wa mtu mwenyewe. Vijiji vyote vya Amani vinashiriki katika programu hizi. Pamoja na kwamba pamekuwepo na malalamiko kuwa wanakijiji wanaojishirikisha zaidi na mambo ya siasa wamepewa programu fulani kwa upendeleo tu, mawanda ya programu hizi sasa yamepanuka kufikia vijiji vyote. Baadhi ya programu hizo ni kama vile:

- **Uvunaji wa mbegu za masambu** (*Allanblackia*): Mradi wa *Tanga Forest Catchment* umekuwa ukishirikiana na kitengo cha UNDP (Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa) cha *Growing Sustainable Business* (Ukuzaji Biashara Endelevu), *International Center for Research in Agro-Forestry* (Kituo cha Kimataifa cha Utafiti katika Kilimo na Misitu), na *Lever UK*, ambayo hununua kiwango kikubwa cha mbegu za mti wa *Allanblckia Stuhlmannii*, ambazo hutumika katika kutengeneza sabuni na mafuta ya kula. Juhudi zinafanywa za kuwezesha upandaji wa mti huu katika hali ya mazingira ya kijijini, ikiwa ni pamoja na upandikizaji ili kupunguza muda wa kukomaa kwake kufikia miaka 5-6. Mapema mwaka 2006 tani 200 zilizovunwa na wakulima 645 zilipatikana; kiasi ambacho kilimpatia mvunaji wa wastani kiasi cha dola za Kimarekeni $400; mapato kwa eneo lote yakiwa Sh Tz. Milioni 300.
- **Ufugaji wa Vipepeo:** Katika mwaka 2005 wakulima 250 walipata pesa taslimu Sh. Tz. Milioni 32 katika programu iliyoanzishwa na *Tanzania Forestry Conservation Group* (Kikundi cha Hifadhi ya Misitu Tanzania) kikisaidiwa na *Conservation International* (kupitia mfuko wa *The Critical Ecosystems Partnership Fund), World Vision, McKnight Foundation*, na wengine. Wakulima huwakusanya na kuwalisha lava wa aina fulani maalumu wa vipepeo mpaka wanapobadilika na kuwa pyupa, ambapo sasa ofisi ya mradi hununua vifukofuko vya pupa hao na kuvisafirisha kwenda kwa wanunuzi huko Marekani na Ulaya, kwa usafiri maalumu wa haraka.
- **Ufugaji Nyuki**: Programu mpya imetoa kwa vijiji mizinga ya nyuki ya kisasa ili kuongeza uzalishji wa asali na nta. Mpaka sasa ni kama mizinga 20 tu ndio iliyokwishategeshwa; lakini inaonekana kuna hamasa ya watu kujiingiza katika shughuli hii.

- **Ufugaji wa Ng'ombe wa Maziwa wa Kisasa:** Mradi mdogo wa uendelezaji wa zao la maziwa umeanzishwa Tanga, kwa msaada wa *Heifer International*. Mradi huu umekuwa ukikuza ufugaji wa ng'ombe wa kisasa wa maziwa, na ukusanyaji wa maziwa katika eneo la Amani. Mpaka sasa kuna vipozaji viwili vya chuma cha pua kisichoshika kutu kwa ajili ya kuhifadhia maziwa, na mamia ya wakulima huleta maziwa kila asubuhi. Kisha maziwa hayo hupelekwa kwenye ushirika wa wakulima wa maziwa, Tanga na huuzwa kwa kampuni ya *Tanga Fresh*, hasa kwa ajili ya kutengeneza mtindi.
- Mabwawa ya Samaki. Mpaka sasa kuna mabwawa ya samaki yapatayo 6 ambayo yanafanya kazi. Mabwawa hayo huzalisha kiasi cha kilo 30 za samaki kila miezi mitatu. Katika vijiji vya Amani protini ya nyama hupatikana kwa kiasi kidogo sana; kwa hiyo samaki wana bei nzuri kwa muuzaji.

**56**. Shughuli nyingine ni pamoja na kuhimiza kilimo cha viungo kwenye mashamba yaliyo nje ya msitu; uzalishaji wa matofali ya udongo mbichi lakini ambayo yameboreshwa, kwa ajili ya ujenzi; mafunzo ya mbinu za kuzuia mmomonyoko wa udongo, hasa katika mashamba ya mazao ya chakula; uwezekano wa kutumia majani ya limao kwenye kontua, kama njia ya kuzuia maji yasitiririke; na nyingine. Aidha, wanafunzi kadhaa waliomaliza shule ambao wanaoishi karibu na nyumba ya wageni ya Amani wamepewa mafunzo ya kuongoza wageni katika eneo hili. Hawa wanalipwa dola za Kimarekani 30 kwa kila siku wafanyao kazi hiyo, ambapo asilimia 20 ya kiaso hicho huenda katika ofisi za HIMAA kwa ajili ya kutengenezea njia za kupitia ndani ya hifadhi. Mwisho HIMAA ina sera inayozingatia kutoa ajira, katika shughuli zake zote, kwa watu wanaotoka katika vijiji vizungukavyo maeneo hayo tu.

**57.** **Ugawaji Ardhi.** Shughuli ndogondogo zilizoelezwa hapo juu ni nyongeza tu inayosaidia kuongeza mapato ya kifedha ya wakulima lakini siyo zenye kuleta pato kubwa kama mashamba ya misituni, na baadhi ya shughuli hizo haziwafikii watu walio wengi. Aidha masoko kadhaa ya shughuli hizo yatafurika baada ya muda si mrefu. Muhimu zaidi ni kupata ardhi mbadala yenye maeneo ya kutosha kuweza kutumiwa kwa ajili ya kilimo, na ambayo yatafidia ardhi iliyochukuliwa na hifadhi ya misitu. Serikali

imeazimia kuhakikisha kuwa ardhi ya namna hiyo inapatikana, ikiwa ni sehemu ya MKUSHUKI.

**58** Mnamo mwezi Machi, mwaka 1999 Wizara ya Ardhi iliamua kuwa ardhi ambayo hapo awali ilikuwa imetolewa kwa ajili ya kilimo cha mkonge, lakini ambayo ama haikuendelezwa kikamilifu au mradi huo haukuwa na mafanikio, irejeshwe katika mamlaka ya serikali za vijiji ili iweze kugawiwa kwa wakulima wa kawaida. Kila kijiji kilitakiwa kutayarisha orodha ya wakulima ambao walitaka kugawiwa ardhi, na Wizara ya Ardhi ikazielekeza Wilaya kuhakikisha kwamba ardhi inagawanywa kwa namna ambayo itaacha barabara za wazi zitakazotumika kusafirishia mazao (taz. Kiambatisho B). Orodha ya mashamba iliandaliwa ikionyesha vijiji ambavyo viligawiwa mashamba hayo. Hakuna hata kijiji kimoja cha Derema kilichokuwa katika orodha hiyo, lakini mashamba ya kwenye mteremko kuanzia vijiji vya Derema yalikuwemo. Mapema Agosti mwaka 2001 Mkuu wa Wilaya ya Muheza aliwaandikia barua Makatibu Tarafa kuhakikisha kuwa ardhi inagawiwa pia kwa wanavijiji vya eneo la Amani; moja ya sababu ikiwa ni kwamba baadhi ya vijiji ambavyo vilipewa ardhi hiyo ya yaliyokuwa mashamba ya mkonge vilikuwa na ardhi yake vyenyewe, kubwa sana. Mkuu wa Wilaya akatoa masharti ya ugawaji mashamba hayo kwa kueleza kwamba kila kipande cha ardhi kinachogawiwa mkulima kilipiwe Sh. Tz. 3,500 ikiwa ni kwa ajili ya usajili na uwekaji mpaka; na kwamba hakuna malipo yoyote ya fidia yatakayofanywa kwa mtu yeyote ambaye atadai kuwa ardhi hiyo ilikuwa mali yake. Ardhi inayozungumziwa hapa iko katika vijiji vya Mkwajuni na Misozwe (taz. Kiambatisho C). Haukupita hata muda wakulima 438 kutoka vijiji saba vinavyozunguka eneo la Amani, viwili kati yake vikiwa vya Derema (Msasa IBC na Kisiwani), wakawa wamekwishajiandikisha kwa ajili ya zoezi hili (taz. Kiambatisho D). Hatuwezi kusema kwa yakini kama hivyo vijiji vingine vitatu viliombewa wakulima waliohitaji mashamba.

**59**. Lakini baada ya kutayarisha orodha hizi na kuzipeleka makao makuu ya Wilaya hakuna lolote la msingi lililofanyika. Wanavijiji wa Derema wanadai kwamba hawakulifuatilia suala hili kwa sababu walikuwa wakisubiri utaratibu wa ulipaji fidia ufanyike. Wanadai pia kwamba hata kama wangekuwa na fedha kidogo za kuwawezesha

kupata mgao wao wa mashamba, hawakuwa na fedha za kuweza kuyaendeleza, na wakahofu kwamba wangeweza kupoteza ardhi yao kama wangeshindwa kuyaendeleza mashamba yao katika kipindi kifupi. Lakini hii haituambii kwa nini wale wanaotoka katika vijiji visivyo vya Derema hawakulifuatilia suala hili; kwani wao walikuwa hawategemei kulipwa fidia ya ardhi wakati huo. Inaelekea kuwa sababu kubwa ya kutokuwepo na matokeo mazuri ya zoezi hili kulitokana na mamlaka yanayohusika hayakuusukuma mchakato huu kwa kuwezesha mawasiliano bayana na ya karibu baina ya wanavijiji na mamlaka ya vijiji yanayodhibiti ardhi iliyotengwa.

**60** Jitihada za mwaka 2001 za kuwashawishi wanavijiji wa eneo la Amani kuhamishia angalau sehemu ya shughuli zao za uzalishaji kwenye maeneo ya nyanda za chini hazikuwa na mafanikio sana. Hata hivyo, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita kumekuwepo na ongezeko la thamani ya ardhi inayolimika katika nyanda hizo za chini. Kutokana na kuendelea kukua kwa uchumi wa Tanzania (na kwingineko Afrika Mashariki) katika miaka mitano iliyopita ardhi iliyo kwenye nyanda za pwani kati ya Dar es Salaam na Tanga imezidi kuwavutia wawekezaji. Soko la mazao kama matunda, karanga, korosho, na maharage linazidi kukua kwa haraka sana. Zao la mkonge, ambalo miaka 30 iliyopita lilikuwa takribani limekufa kama zao la uzalishaji linaanza kufufuka tena na kutumika kwa kutengenezea nyuzi za asili zinazotumika badala ya zile za plastiki, na zao ambalo pia taka zake zinaweza kutumiwa kama biogesi ya kuzalishia umeme. Wakulima wa michungwa wa Tanga wameongeza mapato yao mara nne katika miaka mitano iliyopita, kupitia masoko ya ushirika na ujasiria masoko wanaoufanya huko Nairobi. Upatikanaji wa pembejeo, vitalu vya mimea, mlolongo wa masoko vinaanzishwa kwa kila mojawapo ya mazao haya. Utafiti mpana, utoaji wa pembejeo, mikopo midogo, asasi za masoko na usindikaji, makampuni na miradi mbalimbali vinafanya kazi ya kukiingiza katika soko kilimo cha mazao ya chakula katika Tanzania.

**61.** Kwa ufupi, kuna fursa mpya za uchumi zinazojitokeza katika nyanda za chini. Hii, pamoja na kukomeshwa kwa kilimo cha viungo misituni, inatoa ujumbe wa wazi kwa wakulima wa Derema. Wachache kati yao (kwa mfano wanaotokea Kwezitu hadi Kwemdimu) wamejipatia ardhi kutokana na juhudi zao wenyewe na wanalima

michungwa, minazi, na mahindi. Kinachohitajika kwa wakulima wa Derema walioathirika na hatua zilizochukuliwa na serikali ni kuwa na mpango wa pamoja wa kuufanya uwezekano wa ardhi mbadala liwe jambo linalotekelezeka kikweli kweli, kwa wale ambao wanahitaji ardhi.

**62.** Mojawapo ya makusudio muhimu katika kusimamia Kanda iliyozuiliwa ni kupunguza kuingiliwa kwa Hifadhi ya Mazingira. Ama kuhusu HIMAA, Jambiya na Sosovele wanasema:

> "Ukuzaji wa matumizi ya ardhi ambayo yanadumisha kuwepo kwa wakazi wachache katika maeneo jirani, pengine ndio mkakati wa muda mrefu unaofaa. Lakini, pamoja na kwamba utaratibu huo ndio unaofaa zaidi, tatizo kubwa linakuwa ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya idadi ya watu ikabakia ndogo katika maeneo hayo? ….. Katika maeneo kama ya Milima ya Tao la Mashariki nguvu ya ongezeko la watu ni kubwa"[9]

**63.** Pamoja na kwamba kuanzishwa kwa HIMAA mnamo mwaka 1998 kulieleza kwamba "lengo [la hifadhi] lifikiwe kwa namna ambayo itahakikisha kwamba hali za maisha ya watu haziathiriki na kwamba shughuli zao ……… zina msingi endelevu," nguvu ya kuongezeka kwa idadi ya wakazi wa asili ni suala ambalo litachukua muda mrefu. Mara nyingi suala hili huonekana kama lisiloweza kubadilika, huchukuliwa kwamba watu wanaishi katika eneo fulani huwa wana mizizi ya kale katika eneo hilo, na kwamba kulihama eneo hilo au kuwatafutia eneo jingine ni kuvuruga historia na utambulisho wa watu. Kinyume kabisa na hivyo, maelezo yaliyotolewa hapo juu yanaonyesha kwamba katika Tanzania kwa kawaida,[10] na milima ya Usambara ikiwemo, shuruti za mabadiliko ya kisiasa na masoko zimekuwa zikiendelea "kuandika upya" (kubadilisha) mikakati ya kimaisha ya wanavijiji. Kuanzishwa kwa shughuli za kiuchumi, na pengine baadaye makazi, katika nyanda za chini katika kipindi kisichokuwa na mivutano baina ya majirani, lakini kukiwa na kukinzana zaidi na malengo ya serikali,

---

[9] George Jambiya & Hussein Sosovele, "Conservation and Poverty: A case Study of the Amani Nature Reserve", ***Research on Poverty Alleviation (REPOA) report 0.5, 2001, Dar es Salaam, pg. 13***

[10] Kwa maoni kuhusu Milima ya Usambara Magharibi, taz. Christopher A. Conte, "Colonial Science and Ecological Change: Tanzania's Mlalo Basin 1888-1946," ***Environmental History, April 1999***, Conte anaonyesha jinsi ambavyo vijana katika Karne ya Kumi na Tisa walivyoona tishio katika mfumo wao wa kilimo na kujirekebisha kila ilipobidi: "walionyesha kuwa kwao tayari kufanya majaribio na kuboresha kilimo chao kulingana na mabadiliko ya hali za kiekolojia, kidemografia na kiuchumi. Hakuna mtazamaji yeyote wa Ulaya aliyelekea kuelewa kwamba mabadiliko ya vizazi viwili vya mwasiliano yanawakilisha mwendeleo na kuachana na mazoea ya zamani.

hakuna vurugu zaidi kuliko hali ya kujirudiarudia ya historia ya mwelekeo wa Wasambaa.

**64.** Ikumbukwe kwamba kupatikana kwa ardhi katika nyanda za chini na kugawanywa kwake kwa wanavijiji siyo namna fulani ya mpango uliojificha wa makazi mapya kwa wanavijiji watakaochukua maeneo hayo. Hakuna haja ya kujenga nyumba sehemu nyingine. Ni familia chache tu zitakazoteremka kwenda mbali kidogo na jamaa zao wa karibu. Hakuna haja ya shule za ziada au huduma nyingine za kijamii zitakazohitajika katika maeneo haya mapya, ambayo sana sana yatakuwa na vibanda vya muda vya kukaa wakati shughuli za kilimo zimepamba moto. Mashamba ya Misozwe na Mkwajuni siyo mali au sehemu ya mali binafsi ya vijiji vinavyogawiwa; kwani ardhi waliyopewa ilikwishachukuliwa kwa ajili ya kuendeleza mashamba makubwa, miongo kadhaa huko nyuma kutoka katika ardhi kubwa sana ambayo ilikuwa haijawahi kuwa mali ya mtu yeyote. Hiyo ndiyo sababu Serikali ilichukua hadhari kwa kusema kwamba vijiji jirani vitalipwa tu ada ya kujisajili; na pia ndiyo sababu ikaelezwa zaidi kuwa hakuna fidia itakayolipwa kwa ajili ya ardhi hii kwa mtu yeyote. Kwa kufuata Sera ya Benki, ya Uhamaji usio wa hiari (*Involuntary Resettlement Policy*) haitachukuliwa kwamba kuna “jamii wenyeji” ambao wanapata wawekezaji/ wageni wanaokuja kukaa kwenye eneo lao.

**65.** **Majukumu ya Uongozi**. Jukumu la utekelezaji wa mpango huu wa MKUSHUKI (RAP) limejikita katika asasi mbalimbali ambazo kwa muda wa miaka kadhaa zimekuwa zikifanya kazi pamoja katika kulilinda Tao la Mashariki (Eastern Arc) na juu ya suala la ulipaji fidia. Kwa bahati nzuri asas hizi hufanya kazi kwa karibu sana na zina ushirikiano mzuri. Kazi muhimu za MKUSHUKI ni tatu:

- Kupanga na kulipa fidia, ikiwa ni pamoja na uthibitishaji wa rekodi zilizopo na utunzaji wa mafaili.
- Kuanzisha tena na kufuatilia ugawaji ardhi kwa wanavijiji wa Derema, kwa kuanza na wakulima walioathirika kwa kuchukuliwa mashamba yao, kisha wengine pia.

- Kuhakikisha upanuzi wa “Kanda iliyozuiliwa”, sheria nyingine za maendeleo ya vijijini, shughuli, na marupurupu kwa ajili ya vijiji vya Derema.

**66**. **Malipo ya Fidia**: Kuna hatua kubwa mbili zitakikanazo katika kukamilisha mchakato wa ulipaji fidia. Kwanza mpango huu wa MKUSHUKI pamoja na marekebisho yote yaliyopendekezwa kwenye sera ya zamani ya ulipaji fidia viwekwe wazi kwa wanavijiji wote, na kwa viongozi wa Wilaya na Mkoa. Baada ya kuwa uongozi wa vijiji na watu wote walioathirika wamelazimishwa kukubali mapendekezo mbalimbali ya malipo ya fidia huko nyuma, na baada ya kuwa wamepinga vikali pendekezo la mwaka 2005 la kulipwa asilimia 50, wanahitaji kujua na kutoa maoni yao juu ya mapendekezo yaliyotolewa sasa kwa mujibu wa sera ya Benki ya Dunia yanayohusu mchakato huu. Ili kulitekeleza hili maelezo kuhusu MKUSHUKI yatafsiriwe katika lugha rahisi ya Kiswahili na yaweze kupatikana kwa urahisi. Kisha warsha na maelezo vitolewe kwa vijiji vilivyoathirika. Timu ya WWF ya Tanzania, ambayo inafadhiliwa na taasisi ya *Critical Ecosystems Partnership Fund*, iko tayari kufanya kazi hii. Timu hii iko katika nafasi nzuri ya kuifanya kazi hii, ikizingatiwa kwamba timu hii imekuwa ikijishughulisha na usimamizi na uchunguzaji wa athari za HIMAA kwa muongo mzima.

**67**. Pili, mchakato wa ulipaji fidia lazima ufanyike. Katika hatua hii, TFCMP, ikifanya kazi kupitia ofisi ya *Tanga Catchment Office* ilikwishaweka utaratibu wa malipo wakati wa zoezi la kulipa sehemu ya malipo mnamo mwezi Oktoba mwaka 2005. Maofisa wa FBD, wakishirikiana na maofisa wa serikali za vijiji, watafanya kazi ya kuthibitisha bakaa (fedha iliyobaki) wanayodai wanavijiji, orodha ya malipo yanayodaiwa ikiwa na fomu zilizotiwa sahihi na wakulima. Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa watie saini zao kwenye ratiba (Fomu ya Ardhi Na. 23). Malipo yafanywe kwa hundi, ambazo zitalipwa katika tawi la NMB ya Tanzania, mjini Muheza, ambayo ina akaunti iliyokwishaanzishwa ya ulipaji ya Derema, na ambayo ina halbaki hai. Siku ya malipo inawekwa, na malipo yanafanywa kijiji baada ya kijiji. Baada ya kuhakikisha kwamba hundi ni sahihi, utaratibu wa ulipaji uko sawa, na kuna maofisa wa NMB, Wilaya na wa FBD, thibitisha utambulisho wa mlipwaji na kisha apewe hundi yake. Rekodi ya makabidhiano haya itiwe saini na pande zote mbili na kila upande ubaki na

nakala. Rekodi hiyo ionyeshe kiasi cha malipo yaliyofanywa ikioanishwa na hasara ambayo kwayo malipo yanafanywa, na tarehe ya malipo. Baada ya mkulima kuonyesha kitambulisho chake, Benki ya NMB italipa hizo hundi bila kukata gharama yoyote; lakini wakulima wana hiari ya kuingiza hundi hizo katika akaunti zao nyingine kama wanazo.Timu ya Maendeleo Shirikishi ya WWF inaweza pia kuangalia kazi hiyo.

**68**. **Umiliki wa Ardhi:** Maagizo ya 2001 juu ya ardhi kutoka serikali kuu na wilaya, yaliyoelezwa hapo juu bado yanafanya kazi. Kinachohitajika ni mpango wa dhati wa utekelezaji wa kutembelea maeneo yaliyotengwa kwa wakulima watarajiwa, kushughulikia taratibu zote za maombi na kuhakikisha kwamba mahitajio yote ya kisheria yanatekelezwa. Aidha, mawasiliano na wahusika (wa utafiti, upanuzi wa kilimo, pembejeo) na wanunuzi (vyama vya ushirika, makampuni na watu binafsi) yanahitajika katika maeneo ya vijijini ili kuwawezesha wakulima kuamua mapema ni vitegauchumi gani wangependa kuweka, watahitaji muda gani, watahitaji fedha kiasi gani, na wategemee matokeo gani katika shughuli zao hizo. Kwa mazao mengi ambayo yataweza kuanzishwa katika maeneo mapya, pengine haitakuwa lazima kuhamisha makazi kwenda bondeni, kwenye mashamba mapya; lakini kwa baadhi ya mazao kilele cha kazi za kilimo au thamani kubwa ya zao linalokaribia kukomaa huweza kuhitajia kujenga kijibanda kwenye shamba hilo jipya. Kwa upande mwingine, baadhi ya watu – hasa wakulima vijana ambao wana maeneo madogo ya ardhi vijijini kwao, wanaanza kuwa na familia zao mpya na hawana jinsi ya kufufua mazao ya viungo kwa ajili ya kujipatia fedha – pengine muda si muda watateremka kwenye nyanda za chini na kuanzisha makazi ya kudumu.

**69**. Shughuli hii itahitaji uelekezi wa kitaalamu kwa kipindi cha miaka miwili mpaka zoezi hili liwe limeshika na kueleweka vizuri kwa wale ambao baadaye watachukua nafasi ya kuwaongoza wenzao. Mratibu wa Ulipaji Fidia na Maendeleo (F&M) atapewa mkataba wa kufanya kazi katika ofisi ya mhifadhi wa HIMAA kwa muda wa miaka miwili. Atafanya kazi ya kuwa mtetezi wa wakulima wa Derema – siyo wale tu walioondolewa katika msitu bali pia wanavijiji wengine. Huyu ataanza kazi upesi iwezekanavyo, mara baada ya kuwekwa mkataba baina ya Idara ya Misitu na Ufugaji

Nyuki (IMUN) (FBD) na Benki ya Dunia kwamba itatoa fedha za kulipia fidia na shughuli za maendeleo. Haina maana kuanza kujiingiza kwenye programu yenyewe hasa hadi hapo tarehe za malipo kamili ya fidia zitakapokuwa zimetangazwa katika vijiji: kwani ni wakati huo tu ambapo patakuwa na watu wenye uwezo wa kushughulikia maslahi yao ya wakati huo. Programu hiyo itakuwa na hatua zifuatazo (bajeti ya programu imeonyeshwa hapa chini katika sehemu ya Bajeti ya MKUSHUKI).

*Kielelezo Na.1*

HATUA ZA KUWEZESHA UMILIKI WA ARDHI KATIKA NYANDA ZA CHINI ZA WAKULIMA WA DEREMA

| **Shughuli** | **Mwezeshaji** | **Kuratibu(kwa kushirikiana na)** | **Tarehe** |
|---|---|---|---|
| Thibitisha kwa yakini nia ya dhati ya Wilaya kuhusu ugawaji ardhi, kwa kutoa aula kwa vijiji 5 vya Derema; kubali kwamba wakulima wanaweza kupata hadi mashamba 2 yenye eka tatu tatu | Mratibu wa Ulipaji Fidia na Maendeleo (F & M) katika ofisi ya mhifadhi wa HIMAA | Mkuu wa Mkoa; Mkuu wa Wilaya; Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya; Maafisa Misitu, Ardhi, Serikali za Mitaa, Maafisa Watendaji wa maeneo ya mashamba; na maofisa wenyeji wa vijiji | Anza miezi mitatu kabla ya kuanza kugawa fidia; thibitishia Benki ya Dunia kwa barua za Mkuu wa Wilaya na vijiji wenyeji zinazoonyesha nia ya dhati ya kushghulikia suala hili |
| Wezesha ugawanyaji wa maeneo makubwa ya ardhi katika mashamba yenye eka tatu tatu | Mratibu wa F & M na maofisa Ardhi wa Wilaya na Wizara | Mkaguzi (?), maofisa wenyeji wa vijiji | Anza wakati mpango wa ulipaji fidia uliorekebishwa umekubaliwa na Benki ya Dunia |
| Tembelea kila kijiji kwa maelezo ya awali ya hatua za kuchukuliwa; weka orodha ya wale ambao wanahitaji hasa ardhi | Mratibu wa F & M | Maofisa wa serikali za vijiji katika vijiji vya Derema; wakulima | Anza wakati mpango wa ulipaji fidia uliorekebishwa umekubaliwa na Benki ya Dunia |
| Warsha katika kila kijiji au Makao Makuu ya HIMAA juu ya faida, hasara na gharama za kila moja ya zao la nyanda za chini; ugharamiaji; vyanzo vya akiba, soko (siku 2? ) | Mratibu wa F & M na maafisa mazao/kilimo wa Wilaya | HIMAA, wanunuzi wa mazao na wasindikaji wa mazao katika mkoa wa Tanga, wagavi wa pembejeo; wawakilishi wa miradi na vituo vya utafiti | Anza inapokuwa imethibitika kwamba pesa zote za malipo ya fidia zimekwishaingizwa katika akaunti ya benki ya NMB Muheza |
| Panga safari za basi za wakulima wanaopenda kutembelea sehemu zilizopimwa mashamba | Mratibu wa F & M | Kijiji mwenyeji kinacho-husika; maofisa wa serikali; maofisa wa mazao na ardhi wa Wilaya | Anza wakati mipango ya ugawanyaji wa mashamba inaonyesha mashamba kamili na fedha zimo katika akaunti ya fedha Muheza |
| Ratibu mipango ya maombi kwa ajili ya mashamba na malipo | Mratibu wa F & M | Wizara ya Ardhi, vijiji wenyeji; wengine (?) | Anza baada ya fedha za fidia kulipwa kwa vijiji vilivyoathirika |
| Hakikisha kunakuwepo na utayarishaji na utoaji wa hati za uhamishaji wa mashamba | Mratibu wa F & M | Wizara ya Ardhi; kijiji wenyeji; usajili wa ardhi | Baada ya maombi kukubaliwa |
| Hakikisha kwamba taarifa kuhusu chakula cha kilimo, pembejeo na masoko | Mratibu wa F & M, na wadau wote | Wizara ya Kilimo; miradi ya wafadhili | Uwiano wa miaka miwili ya mkataba wa Mratibu wa F & M |

| | | | |
|---|---|---|---|
| zinatolewa katika wakati ufaao | | | |

**70**. **Kanda iliyozuiliwa na Njia Mbadala za Maisha:** Mratibu wa F & M atafanya kazi chini ya Mhifadhi Mkuu wa HIMAA, ambaye tayari ana naibu wake anayeshughulikia Utafiti, Mafunzo na Maendeleo ya Jamii. Baadhi ya shughuli hizo huendeshwa kwa msaada wa washiriki wengine wa nje, lakini naibu mhifadhi ndiye mwenye madaraka kamili kuhusu kiwango na idadi ya mikutano inayoongezeka na utafiti katika HIMAA. Mratibu wa F & M atakuwa katika nafasi nzuri ya kushiriki katika majukumu mbalimbali yanayohusu Maendeleo/Maisha ya Jamii. Ataratibu, akisaidiwa na washiriki anuwai wa shughuli ndogondogo za kijamii katika eneo linalozunguka Amani (ikiwa ni pamoja na wale wapendeleao kuanzisha miradi mipya, ambapo wengi hupendelea kutumia mazao ya misitu yasiyo ya mbao (NTFP) (k.m. aina za kombamwiko, mimea ya dawa za kienyeji) kama vile ya masambu, ambayo yana uwezekano wa kuwa na matokeo geu kwenye HIMAA yenyewe. Kwa namna hiyo atasaidia kusimamia vipengele vya maendeleo vya uhusiano kati ya kanda iliyozuiliwa na vijiji.

**71.** **Ushirikishwaji wa Jamii**. Maendeleo shirikishi yamekuwa ni jambo la kuzingatiwa katika mabadiliko ya njia za hifadhi katika maeneo ya Usambara Mashariki tangu mwanzo. Shughuli za Wafini katika eneo hili hadi kufikia miaka ya 1980 zilikuwa bado zimekitwa katika shughuli za misitu ya kibiashara. Mashinikizo kutoka Ufiini na kwa wataalamu wa hifadhi na makundi mbalimbali katika Tanzania yalizifanya shughuli za Kifiini katika eneo hili zielekee zaidi kwenye hifadhi ya kiekolojia; na kuanzia mwaka 1992 IUCN ikashuhudia kuanzishwa kwa Mradi wa Hifadhi ya Usambara Mashariki na Maendeleo ya Kilimo ambao ulifadhiliwa na Ufiini na Ulaya (EUCADEP, baada ukajulikana kama EUCAMP) kama jaribio la kushirikiana katika kulinda ubioanuwai pamoja na kutambua mahitaji ya watu. Tathmini ya Ushirikishwaji wa Jamii ya Vijijini ilitumiwa kuweka mipango ya vijiji 16 vya kanda iliyozuiliwa kuzunguka HIMAA ilipoanzishwa mwaka 1998 na kuanzisha baadhi ya shughuli za mashambani ambazo

zilisaidia shughuli za hifadhi. Bodi ya ushauri kwa ajili ya HIMAA ilianzishwa ikiwa na wadau mbalimbali kama wajumbe, ikiwa ni pamoja na maafisa wa serikali, makampuni ya chai, na wawakilishi wawili wa jamii inayozunguka eneo hilo (hata hivyo Bodi hiyo haikuwa inakutana mara kwa mara). Suala la Ushoroba wa Derema lilipoanzishwa PRA ilishauriana na vijiji vitano ambavyo vilikuwa viathirike; kukawa na matokeo ya muda ya vijiji kulikataa wazo la hifadhi za msitu ya vijiji kuwa ndicho chombo cha kusimamia Derema.

**72**. Ilipoamuliwa kuitangaza Derema katika Gazeti la Serikali kama sehemu ya hifadhi ya Taifa, na hivyo basi, kuondoa mashamba yote yaliyokuwa yakilimwa, kulikuwa na mawasiliano na wanavijiji wakati wote. Tathmini ya athari za kijamii, ambayo imetolewa mapema katika maelezo haya, ilitoa maelezo mapana kuhusu mradi wa Derema na athari ambazo zinawahusu wale ambao wataathirika nao. Uwekaji mpaka ulifanywa kwa kushirikiana kikamilifu na wanavijiji, ambao wenyewe walifanya kazi ya kulifyeka eneo hilo, iwapo walikuwepo walioathiriwa moja kwa moja na zoezi hilo walilipwa fidia. Uwekaji hesabu na orodha ya mazao ulifanya kuwepo na mawasiliano ya moja kwa moja kati ya wanavijiji, mamlaka za vijiji, maafisa Wilaya na Watathmini.

**73.** Kuanzia katikati ya mwaka 2002 hadi katikati ya mwaka 2006, yaani kuanzia wakati tathmini ilipofanywa hadi kufikia wakati ambapo ripoti hii iliandikwa kulikuwa na mawasiliano ya vipindivipindi baina ya wanavijiji na mamlaka yanayohusika na zoezi hili, huku hali ikiongezeka kuwa nyeti. Timu huru ya ukadiriaji ilitembelea HIMAA na maafisa wa serikali katikaTanga na Muheza mnamo mwezi Februari mwaka 2003, katika utekelezaji wa kazi yao, lakini hawakufanya mikutano yoyote na wanavijiji. Mnamo mwezi Juni 2004 ujumbe wa Benki ya Dunia, wa usimamizi wa TFCMP (timu kubwa, ikiwa inajumuisha UNDP, Danida, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Ufiini, NORAD, WWF na maafisa kadhaa wa ngazi za juu wa Tanzania) ulitembelea eneo hilo na wakajionea wenyewe, pale Msasa IBC, jinsi wanavijiji walivyokuwa wamekasirishwa na ucheleweshwaji wa malipo. Kufikia Juni 2005 washauri wa WWF walikuwa wakiwaeleza maafisa wa Mkoa na Wilaya juu ya hasira na kutafrika kwa wanavijiji, na jinsi thamani ya ulipwaji fidia ilivyoamuliwa. Jamii zilikuwa pia na wasiwasi….. iwapo itatokea kukapatikana fidia toshelevu.

**74**. Mnamo mwezi Agosti 2005, Wizara ya Ardhi ilipokubali kuongeza pesa ya kutosha kwenye akaunti ya kulipia fidia Derema ili kuwezesha kulipa nusu ya malipo. Ofsi ya Misitu iliyoko Tanga ilianza kufanya kazi ya kuhakiki orodha ya mazao na kupata sahihi za wakulima kuonyesha kwamba fedha ambayo wangelipwa ilikuwa halali. Hali katika kipindi hicho ikageuka kuwa ya wasiwasi sana. Wakulima wakaanza kudai riba kwa kipindi cha miaka mitatu ambayo ilipita, tokea tathmini ilipofanywa; mbaya zaidi wakakataa thamani ambayo mazao yao yalipewa. Katika kijiji cha Kwezitu watu waliokuja kuthibitisha thamani iliyokadiriwa kwa mazao yao walikuwa chini ya asilimia 50. Huko Msasa IBC wanakijiji waliilazimisha timu iliyokuwa inafanya zoezi la kutathmini mazao kuacha zoezi hilo; hadi ilibidi timu hiyo iokolewe na polisi. Katika kijiji cha Kambai hakuna hata mkulima mmoja aliyejitolea kwenye zoezi hilo. Barua kutoka kwa wanavijiji zilitoa malalamiko juu ya thamani ambazo mazao yao yakuwa yanapewa, pamoja na suala la riba; kiasi kwamba Mbunge wa Wilaya ya Muheza na Mkuu wa Wilaya wakaingilia kati na kufanya mawasiliano na Wizara ya Maliasili na Utalii, na pia kuwatuliza wananchi. Ikakubaliwa kwamba malipo yakubaliwe na wanavijiji, lakini isichukuliwe kwamba malipo hayo yalikuwa yanawakilisha asilimia 50 ya malipo yote. Kwa wale wakulima ambao malipo yao yote yalikuwa kidogo sana ikashauriwa kwamba yalipwe yote kwa kutumia hundi moja; lakini wakulima wakang’amua kwamba huenda wangeweza kuchukuliwa kwamba wangekuwa wamelipwa kikamilifu. Kwa hiyo, wakadai nao walipwe kama wengine na waendeleze mapambano yao. Uthibitishaji wa mahesabu ukakamilika katika kituo cha sehemu ya kati kutoka vijijini (Kituo cha Zigi, lango la HIMAA). Katika sehemu hiyo na pia wakati malipo yalipofanywa Muheza kulikuwa na askari wa kulinda usalama.

**75**. Kazi ya uwandani kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huu ilifanyika katikati ya Juni, 2006. Kila kijiji kilitembelewa na kupewa maelezo marefu na ya kina kwamba serikali ilikuwa imeomba msaada kutoka mradi wa misitu wa Benki ya Dunia ili kuweza kutatua suala la muda mrefu, la ulipaji fidia. Wanavijiji walitoa malalamiko yao kuhusu hali iliyokuwa imetokea na kuelezea athari za hasara zao kwa kipindi cha miaka mine toka mazao yao yalipohesabiwa na kuachwa. Wakaelezea matarajio yao mema katika

kupata suluhisho la hali hiyo. Katika kijiji kimoja kulikuwa na tukio la kutupiwa mawe mojawapo ya magari yaliyokuwa yanatembelea vijiji; lakini tukiacha tukio hilo mikutano iliendeshwa vizuri na wanavijiji walishiriki kikamilifu.

**76**. **Mbinu za Kushughulikia Malalamiko**. Sera ya Benki ya Dunia inahitajia kwamba pawepo na utaratibu wa kuweza kutatua migogoro ambayo inaweza kutokea katika kipengele chochote cha mchakato wa ulipaji fidia na masuala ya maendeleo. Utaratibu huo uweze kuwa rahisi na usiwe na mizengwe, na kwamba awepo mtu wa tatu , mbali na pande hizo mbili, wakati wa shughuli hizo. Kama ilivyokwishaelezwa, katika Derema kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kuhusu namna shughuli ya kuhesabu mazao ilivyofanywa. Patahitajika kuwapo na juhudi kubwa za masikilizano baina ya mamlaka na wanavijiji ili kuweza kupata utatuzi wa tatizo lililopo hivi sasa; haitarajiwi kwamba haja ya kutaka kumaliza utekelezaji wa suala hili itatosha kuondoa malalamiko yote.

**77**. Kwa kuwa kwa kiasi kikubwa inakubalika kwamba hesabu za mazao zilikuwa sahihi na za kuridhisha, haitarajiwi kwamba kutakuwa na malalamiko mengi kuhusu hesabu hizo za mwanzo. Migogoro inayoweza kutokeza ni ile ambayo itakuwa imesababishwa na (a) kutokuwepo kwa rekodi zote za shamba (b) mgawanyo wa mimea katika kategoria mbalimbali na ubora wa utunzaji wa zao hilo, (c) thamani iliyowekwa kwa kila aina ya kategoria ya zao linalohusika. Kati ya haya kunaweza kuwepo na kesi chache za rekodi zisizoonekana (kipengele (a)), na kwa kupitia vizuri majedwali, fomu za rekodi, na picha inawezekana kuyaondoa matatizo haya pasi na kuhitaji michakato mikubwa ya kusuluhisha migogoro. Kipengele cha (b) ni suala ambalo hakuna ushahidi mbadala uliowekwa na wafanya tathmini (hakuna picha za kila mti au mmea, na haielekei kwamba wanavijiji wanaweza kuthibitisha kimaandishi kuwa mimea yao ilikuwa katika hatua kubwa ya ukomavu wake au ilikuwa inatunzwa vizuri zaidi kuliko inavyoelezwa katika kategoria za wafanyatathmini, ambazo ziliwekwa mara tu baada ya kumaliza mahesabu ya shamba). Katika kusambaza matokeo ya mchakato huu wa MKUSHUKI, watekelezaji wa MKUSHUKI wanatakiwa waonyeshe kwamba hapatakuwepo na uwezekano wa kurudia kufanya marekebisho labda kama ushahidi wa wazi utaonekana.

Mwisho, kipengele (c) ni suala pana la MKUSHUKI, na litachukuliwa kuwa limeshughulikiwa wakati wa kupitishwa kwa MKUSHUKI na kufikishwa kwa wanavijiji walioathirika.

**78**. Kwa ufupi, kesi za migogoro zinatakiwa kuwa chache sana, hata kama kwa ujumla kumekuwa na kutokuridhishwa na ucheleweshaji katika suala zima. Mpango huu utakapopitishwa na mikataba ya fidia ya kila mtu kutiwa saini, wale wanaohusika wataarifiwa katika mikutano ya vijiji juu ya utaratibu utakaofuatwa katika kutoa malalamiko na kutaka kufanyiwa marekebisho. Utaratibu wa kutoa malalamiko utakuwa rahisi, ukianza kushughulikiwa katika ngazi ya kijiji ili kuharakisha mambo, nyumbufu, na utakuwa tayari kupokea ushahidi mbalimbali, lakini ukizingatia haja ya kutocheleweshа mambo; utakuwa wa haki na utatoa utatuzi usio na upendeleo. Mchakato wa kutatua malalamiko utakuwa kama ifuatavyo:

**79**. Mratibu wa Fidia na Maendeleo (F & M) atafungua mafaili ya kesi zote, ambayo yatakuwa na nakala za mahesabu halisi ya mazao na fomu za madai, picha halisi zilizochukuliwa wakati wa zoezi la tathmini, na mafaili ya Ekseli ya fidia inayopaswa kulipwa. Atakuwa tayari kuzipitia rekodi hizi za wakulima, mmoja baada ya mwingine.

**80**. Mratibu wa F & M atapokea malalamiko, ya kimaandishi, juu ya sehemu yoyote ya mchakato ambayo inamhusu mkulima anayehusika. Atatoa maelezo kulingana na data alizonazo, lakini pia, ikibidi, atamweleza mlalamikaji kwamba malalamiko juu ya idadi ya mazao, uanishaji wa mazao au thamani yake vitahitaji ushahidi maalumu na dhahiri.

**81**. Pale ambapo ushahidi unatolewa mratibu wa F & M ataitisha kikao baina yake, akiwa mshauri, mamlaka ya kijiji cha mlalamikaji, na mlalamikaji mwenyewe, ili kutafuta suluhisho. Mamlaka ya kijiji yanaweza kuwaita watu na mashahidi wengine watakaosaidia katika kuzipitia upya taarifa za kesi hiyo: hatua hii itazingatia utatuzi wa malalamiko na migogoro uliokitwa katika taratibu za kijadi za eneo linalohusika. Mamlaka ya kijiji yatatoa maamuzi yao kwa maandishi kulingana na maoni yao, na

nakala ya maamuzi hayo atapewa mratibu kwa utekelezaji au kwa kuyapeleka kwa watu wengine ambao watahitaji kulifuatilia suala hilo ili kuridhisha maamuzi ya mlalamikaji.

**82**. Iwapo mlalamikaji atakuwa hajaridhika na maoni ya wengi wa maafisa wa kijiji anaweza kukata rufaa kwenye Wilaya. Mratibu atapanga mkutano wa Afisa Ardhi na Afisa Mazao, chini ya uenyekiti wa Katibu Mtendaji wa Wilaya au mteule wake. Mratibu atapanga mkutano wa Afisa Ardhi na Afisa Mazao, chini ya uenyekiti wa Katibu Mtendaji wa Wilaya au mteule wake. Kikao hiki kinaweza pia kuita mashahidi wengine. Kikao kitatoa maamuzi yake kwa maandishi, na kutoa nakala kwa mlalamikaji na Mratibu, ambaye atalifuatilia suala hili iwapo kuna hatua zozote zinazopaswa kuchukuliwa.

**83**. Maamuzi yoyote mazuri yatakayoangukia upande wa mlalamikaji yatatakiwa kutekelezwa katika kipindi cha miezi miwili, au mwezi mmoja kama uamuzi ni suala tu la kulipwa pesa. Iwapo mlalamikaji hatakuwa ameridhika na maamuzi ya kamati ya Wilaya anaweza kulipeleka suala lake mahakamani. Taarifa zote za vikao hivyo zitatunzwa na ofisi ya ardhi ya Wilaya na Mratibu wa F & M kwa ajili ya HIMAA.

**84**. Taratibu hizi zitapitiwa baada ya kipindi cha mwaka mmoja tangu kuanza kwa malipo ya mwisho ya fidia. Bodi ya Ushauri ya HIMAA, ikiwa pamoja na wenyeviti na makatibu wa vijiji watapewa taarifa na Mratibu wa F & M juu ya ubora au ubovu wa utaratibu wa kushughulikia malalamiko, na itachukua hatua zitakikanazo kama kutakuwa na haja.

**85**. **Usimamizi na Tathmini ya MKUSHUKI**. Mipango hii ya usimamizi wa MKUSHUKI itaratibiwa na mipango ya jumla ya usimamizi na tathmini ya TFCMP. Mfumo wa kuendeshea usimamizi huu unafanywa udurusu kwa sasa. Lengo la mipango ya usimamizi litakuwa ni:

- Kuhakikisha kwamba fidia zote zinazopaswa kulipwa zinalipwa katika kipindi cha miezi sita baada ya kupitishwa kwa shughuli hii, ikiwa ni shughuli ya ziada ya TFCMP

- Kuweza kutoa taarifa, wakati wowote, juu ya malalamiko ambayo yameletwa na ama yanashughulikiwa au yametatuliwa
- Kuhakikisha kwamba mchakato wa kupata na kugawa ardhi katika nyanda za chini unafanywa kwa haraka na kwa makini kwa wakulima wa Derema waliotayari kugawiwa.
- Kuchukua hatua, kwa kushirikiana na kituo cha HIMAA, za kufanya tathmini ya mwisho ili kuona kama watu walioathirika kwa kuchukuliwa kwa ushoroba wa Derema wameweza au wanaelekea kuweza kurejesha uwezo wao wa kimapato na hali zao za maisha ya awali[11].

**86**. Katika suala la kufuatilia matumizi ya fedha za fidia na maendeleo, baadhi ya viashirio muhimu vya utendaji, vinavyothibitika, ni hivi vifuatavyo. (Mratibu wa F & M atasimamia mfumo wa kuvifuatilia viashirio hivyo kwa muda atakaokuwa na mkataba. Baada ya hapo mfumo huo utasimamiwa na Mhifadhi Mkuu wa HIMAA)

- Akaunti za malipo ya fidia, kwa idadi na asilimia ya malipo yote yatakiwayo kulipwa
- Malalamiko yote yatakayotambuliwa kuwa ni halali, na ambayo yamekwishatatuliwa, kwa idadi na asilimia ya malalamiko yote yaliyoletwa
- Orodha ya wakulima walioathirika na wengine katika vijiji vya Derema ambao wanataka mashamba katika nyanda za chini, na idadi na asilimia ya wale ambao wanapata vibali na wanaanza kuyaendeleza mashamba yao
- Idadi ya mashamba ya namna hiyo ambayo yako tayari kusajiliwa, yale yaliyosajiliwa kama yamechukuliwa na wakulima wa Derema walioathirika, wakulima wengine wa Derema, na wakazi wengine wa kanda iliyozuiliwa ya HIMAA, na wengineo.

[11] Ili kuanza mfumo wa muda mrefu wa ufuatiliaji mratibu wa F&M ataongeza mafaili kwenye rekodi za malipo ya fidia, ambazo zitatumika kufuatilia matumizi ya fedha za fidia kwa ajili ya kujishughulisha na shughuli nyingine zenye kuongeza mapato; kwa mfano, kununua ardhi nyingine, iwe ni kwenye nyanda za chini zilizochaguliwa au sehemu nyingine, katika miradi ya jirani na eneo lililozuiliwa katika HIMAA, au katika shughuli mpya ya kibiashara . Ni wazi kwamba hakuna mahali maalumu pa kuanzia kwa ufuatiliaji wa kesi zote za watu walioathirika, lakini inawezekana kupata taarifa ya kutosha kuweza kuelewa nini watu walioathirika wanaweza kufanya kufidia mashamba yao ya viungo/matunda katika Derema.

- Orodha ya vitegauchumi vinavyofahamika katika mikakati ya kujipatia riziki ya ziada, kwa aina na mahali walipo wale wapatao fidia ya ShT <200,000; 200,000; <500,000; 500,000; <milioni 1; >milioni 1.
- Idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika shule za sekondari kutoka familia za vijiji vitano vya Derema, kabla na baada ya kulipwa fidia.
- Tofauti za kijinsia katika majibu ya uchunguzi uliofanywa kabla na baada ya masuala ya malipo ya fidia
- Hatua nyingine, kama zitakavyoelekezwa katika warsha kuhusu suala hili au zitakazoelekezwa na timu inayofadhiliwa na WWF ambayo imefanya uchunguzi mara mbili wa Athari za Kijamii katika eneo la Derema.

**87.** **Ratiba ya Utekelezaji**. Ratiba ya utekelezaji wa MKUSHUKI inategemea upatikanaji wa fedha katika kushughulikia programu ambazo tayari zimesanifiwa kutekelezwa. Inategemewa kwamba fedha zitapatikana kwenye mwezi Novemba 2006, lakini ratiba ifuatayo inaainisha hatua katika programu hiyo bila kuzingatia tarehe maalumu na kuanza kwake.

*Kielelezo Na 2*

RATIBA YA UTEKELEZAJI WA MKUSHUKI

| **Tarehe** | **Shughuli** | **Matarajio ya kitakachofanyika** |
|---|---|---|
| Mwezi 1 | Ajiri Mratibu Uhamaji na Maendeleo (MUM) | Utambuaji wa wahusika umekwishafanywa mara tu baada ya MKUSHUKI kupitishwa; magari na vifaa vingine viwepo kuwezesha kazi kuanza. |
| Mwezi 2 | 1) Thibitisha ratiba ya malipo na kiasi cha malipo ukitoa kiasi kilicholipwa katika 2005 kwenye jumla ya kiasi kinachodaiwa<br>2) Hamisha fedha zote kwenda katika akaunti ya malipo ya fidia, Muheza<br>3) Tangaza katika kila kijiji programu ya malipo mapya/ya mwisho | TFCMP inatoa wafanyakazi kushughulikia ratiba hadi Mratibu Uhamaji na Maendeleo atakapoanza kushughulika.<br><br>Uhamishaji wa fedha unafanywa bila kuchelewa<br>MUM na Wasimamizi wa WWF kutembelea vijiji, pamoja na kusambaza utaratibu mpya na kujibu maswali |
| Mwezi 3 | 1) Tangaza programu, tembelea vijiji kutia sahihi mikataba ya mwisho na walipwa fidia<br>2) Mwisho wa mwezi, fanya malipo | Wanavijiji wamekubali programu ya mwisho. Hundi zinalipwa kutoka benki ya Muheza, zinalipiwa Muheza kwa fedha taslimu au kwa mtindo wa “benki inayotembea” kama inavyofanyika kwa Songo Songo |
| Mwezi 4 | MUM anafanya kazi katika vijiji husika | Wanavijiji wa maeneo mapya wamethibitisha |

| | | |
|---|---|---|
| | na mamlaka ya wilaya kubainisha ardhi ambayo watapewa wakulima wa Derema | kukubai kwao mipango ya serikali, ya muda mrefu, ya kugawa tena mashamba ambayo hayajatumika |
| Mwezi 5 | 1)Wakulima wanaanza ziara<br>2)Wataalamu (mazao na mashamba) wanatembelea vijiji 5 vya Derema kutoa mafunzo kuhusu aina za mazao yanayowez kulimwa kwenye nyanda za chini | MUM keshafanya mipango ya usafiri na ratiba ya ziara hizo<br><br>MUM amekwishafanya mawasiliano na wataalamu wa kilimo na sekta binafsi ambao watatoa mafunzo juu ya aina mbalimbali za mazao yanayoweza kulimwa, na vitega-uchumi vinavyoendana na stadi za wakulima, mapendeleo yao na uwezo wao |
| Miezi 6-12 | 1) Ziara za wakulima, ununuzi wa ardhi unaendelea<br>2) miradi mbadala ya kupatia riziki na upanuzi wa mashamba vinaendelea | Uhamishaji wa ardhi unamalizika , pamoja na hati zinazohusika kupitia Wilaya na Mkoa. |
| Miezi 12-24 | 1) usimamizi unaanza na unaishia na uandishi wa ripoti<br>2) Mimea inapandwa, mavuno ya kwanza katika nyanda za chini yanavunwa | Mkataba umekubaliwa na WWF kufanya usimamizi na uchunguzi wa matokeo<br>Wakulima wamechukua mashamba mapya, wamelima na kupanda bila bugudha ya aina yoyote |
| Mwezi 24 | MUM anamaliza kazi kwa kuandika ripoti | Mamlazaka za wilaya zimeingiza programu hii katika programu zao za kawaida, wanaendelea kutoa huduma kwa wakulima.<br>HIMAA inachukua jukuma la mahusiano na vijiji 5 vya Derema kama wafaidikaji wa miradi mbadala ya kupatia riziki, na kama vijiji vishirikishwaji katika mgawanyo wa mapato |

**88. Bajeti kwa ajili ya Utekelezaji wa MKUSHUKI**. Sehemu kubwa ya bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa MKUSHUKI, kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali 5 hapa chini, ni ile ya malipo ya fidia. Lakini mbali na kipengele hicho fedha inahitajika kuendeshea MKUSHUKI, kuhakikisha kwamba malipo ya fidia yanafanywa, na kuanzishia Ofisi ya Malipo ya Fidia na Maendeleo, chini ya Mratibu ambaye naye atawezesha shughuli nyingine za lazima katika kuikamilisha kazi hii, ikiwa ni pamoja na uwezeshaji muhimu utakaofanywa na Serikali ya Wilaya ya Muheza. Majedwali yafuatayo mawili yanaonyesha vyanzo vya fedha kwa ajili ya ulipaji fidia na mgawanyo wa fedha katika bajeti yote. (Ifahamike kwamba mchango wa Serikali ya Ufini haujatolewa kwa miaka kadhaa, na hakuna hakika kwamba utatolewa).

## RASIMU

*Jedwali 4*

VYANZO VYA FEDHA (katika US $)

| | **Wakati** | **Chanzo cha Fedha** | **Kipindi cha Kazi (miezi)** | **Mwaka wa 1** | **Mwaka wa 2** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Matayarisho** | | | | | | |
| Rekebisha uchunguzi wa kijamii kulingana na hali iliyopo | Nov. 05 - Juni 06 | CEPF / WWF | 2 | 30,000 | | 30,000 |
| Kutayarisha MKUSHUKI | Mei 06 – Agost 06 | FBD kutoka TFCMP | 2 | 50,000 | | 50,000 |
| **Malipo ya Fidia** | | | | | | |
| Malipo ya Fidia | Mei 2006 | *Global Conser-vation Fund* | | 350,000 | | 350,000 |
| Malipo ya Fidia | Aprili/Mei 2005 | Serikali ya Ufini | | 200,000? | | 200,000? |
| Malipo ya Fidia | Aprili/Mei 2005 | Serikali ya Tanzania | | 95,000 | | 95,000 |
| Malipo ya Fidia | Oktoba 2006 | WB/TFC MP | | 1,459,261 | | 1,459,261 |
| **Uongozi** | | | | | | |
| Taz. Jedwali lifuatalo | | WB/TFC MP | | 104,600 | 86,000 | 190,600 |
| | | | | | | |
| JUMLA | | | | 2,288,061 | 86,000 | **2,374,061** |

*Jedwali 5*

BAJETI YA UTEKELEZAJI WA MKUSHUKI

| **Kitu/shughuli** | Muda | Miezi | $/mw | Mwaka 1 | Mwaka 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mpango wa usimamizi shirikishi | 2006 – 2008 | 8 | 10,000 | 10,000 | 40,000 |
| **Gharama za Uongozi** | | | | | |
| | | | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Mratibu wa MKUSHUKI | 2006 – 2008 | 24 | 1,500 | 18,000 | 18,000 |
| Vifaa vya Ofisi katika HIMAA | 2006 – 2008 | 24 | 250 | 3,000 | 3,000 |
| Gari (4 x 4) + PLM x 24 | 2006 – 2008 | 24 | 1,000 | 37,000 | 12,000 |
| Mwasiliano | 2006 – 2008 | 24 | 400 | 4,800 | 4,800 |
| Pikipiki 5@ $3,000 kuwawe-zesha maafisa wa Wilaya ya Muheza: Ardhi, Mazao, Misitu, Utawala, na PLM | 2006 – 2007 | 24 | 400 | 19,800 | 4,800 |
| Uwezeshaji wa serikali za vijiji vya Derema katika zoezi la Ugawaji ardhi na ulipaji fidia | 2006 – 2008 | 24 | 1,000 | 12,000 | 12,000 |
| **Fidia** | | | | | |
| Kiasi kinachodaiwa | 2006 – 2007 | 8 | | 2,184,261 | |
| **JUMLA** | | | | **2,288,061** | **86,000** |
| **JUMLA KUU** | | | | **$ 2, 374, 661** | |

## KIAMBATISHO 1a

**Mchanganuo wa kina wa mapato kwa kila fungu au zao uliochukuliwa moja kwa moja kutoka katika utafiti uliofanywa na *Proper Consult,* pamoja na baadhi ya mabadiliko kwenye zao la kwanza, Iliki, na uhariri wa sura ya jedwali lote.**

### 1.0 ILIKI

Mapato ya jumla: (kwa kila fungu k.mk @ kilo 3 zilizokaushwa kw. mw….. 7,200/=

Kutoa: Gharama za Uendeshaji @ 40% (taz. chini) ……………………….. 2, 800/=

Mapato Halisi kwa mwaka 3-6 ……………………………………………...4, 320/=

Mapato Halisi kwa miaka 6 – 12 ni 20% ya mapato yaliyotangulia au 864/=

## RASIMU

Thamani ya zao ………YP*NI 4,320/=) kwa miaka 3 ya kwanza + YP*NI (86/=) kwa miaka 6 inayofuata (Tarakimu iliyopatikana ni makadirio kulingana na thamani ya mtaji, angalia mwisho wa Jedwali hapa chini)

Kiwango cha uwekaji mtaji, (i), kilichochukuliwa ni 4.5%, yaani kiwango, katika Tanzania, kichukuliwacho kuwa hakina hatari.

**M 1 (zao lililokomaa, daraja la kwanza) ….. zao safi na lenye mafungu yaliyotunzwa vizuri**

Tukichukulia kwamba:

Shamba lililotunzwa vizuri, matumizi mazuri ya ardhi, za kutoa mavuno mengi

Idadi nzuri ya mimea, uachaji nafasi mzuri kati ya mimea, wa sentimeta 2.5 x 2.5

Kilimo kisichochanganya mazao; zao la iliki peke yake

Lenye kutoa mavuno yanayovuka 80% (chanzo: utafiti)

Ni mashamba machache sana yanayofikia kuwa na sifa hizi za M1, yanapatikana katika baadhi ya sehemu za Msasa IBC na Kwemdimu.

**Kwa hiyo M1 = 5,100/= kutokana na vigezo vilivyoelezwa hapo juu.**

**M2 (zao lililokomaa, daraja la pili): Thamani ya zao imewekwa kwenye kiwango cha 65% ya M1, ambayo ni 3,315/=**

(a) Wastani wa Uzalishaji 60% - 80%

(b) Utunzaji wa shamba wa kuridhisha

(c) Wastani wa matumizi mazuri ya ardhi 60% - 80%

Mambo yaliyotajwa hapo juu yanaleta kama 65%

**M3 (zao lililokomaa, daraja la 3): Thamani ya zao imewekwa kwenye kiwango cha 40% ya M1, au 2,040/=**

(a) Uzalishaji wa Chini ya wastani, kati 40% - 60%

(b) Utunzaji mbaya wa iliki, 40% - 60%

(c) Shamba halikutunzwa vizuri (lina mapori), 40% - 60%

(d) Shamba la zamani lililotelekezwa, 40% - 60%

Mambo yaliyotajwa hapo juu huleta kama 40%
(Mashamba mengi ya Kisiwani yamo katika kundi hili)

**MICHE NA/AU MITI MICHANGA**

**S1: (daraja la kwanza):** Miche ya iliki ambayo ni ya miezi 4-6 huwakilisha kama 10% ya thamani ya zao la (M3), katika uwekaji vitegauchumi, gharama, n.k., sawa na Sh.T 204.

**S2 (daraja la pili):** Miche ya iliki ambayo ni ya wiki 6 -12 huwakilisha 5% ya ………..

**KIAMBATISHO 1b**

**USHOROBA WA MSITU WA DEREMA ULIOPENDEKEZWA**
**MATRIKI YA MAPATO YA MAVUNO YA DEREMA 13 7 02.xls pamoja na marekebisho ya iliki**

**TATHMINI YA MALIPO YA FIDIA KWA MAZAO YA SHAMBANI**

| | Zao (fungu) | Lipa fidia kwa kila | Umri wa mzunguko9 (myk) (kupanda hadi kukomaa) | Mara za kuvuna kwa mwaka | Jumla ya mavuno kwa mwaka (kg au vipande)/ fungu | Bei kwa kg/kimoja katika Sh.Tz. | Mapato ya Jumla/ fungu kwa mwaka | Gharamaza uendeshsji kwa mwaka ktk % | Pato Kuu la mwaka/fungu | Matumizi ya Nyumbani | Pato Halisi /fungu kwa mwk katika Sh.Tz. | Pato Halisi /fungu kwa mwezi ktk Sh.Tz. | THAMANI YA MAZAO (YP X NI = CV) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Iliki | kilogramu | 3 | 3 | 3 | 2400 | 7,200 | 40% | 4,320 | 0% | 4,320 | 360 | 5,100 | 3,315 | 2040 | 204 | 102 | 51 |
| 2 | Pilipili manga | kilogramu | 3 | 2 | 2.5 | 1,000 | 2,500 | 40 | 1,500 | 20 | 1,000 | 83 | 2,900 | 1,160 | HH | 116 | 6 | *3* |
| 3 | Migomba | mikungu | 1 | 3.5 | 8.0 | 600 | 4,800 | 30 | 3,360 | 35 | 1,680 | 140 | *3,920* | 3,080 | HH | 11.2 | 224 | 6 |
| 4 | Kahawa | kilogramu | 2 | 1.0 | 3.0 | 140 | 420 | 35 | 273 | 0 | 273 | 23 | HH | 1,336 | HH | 53 | HH | 2 |
| 5 | Mdalasini | kilogramu | 2 | 0.5 | 3.0 | 530 | 1,590 | 40 | 954 | 20 | 636 | 53 | 1,776 | 1,065 | HH | 7 | HH | 2 |
| 6 | Karafuu | kilogramu | 3 | 1.0 | 7.0 | 2,500 | 17,500 | 45 | 9,625 | 15 | 7,000 | 583 | 60,000 | 36,000 | HH | 2400 | HH | 60 |
| 7 | Mananasi | idadi | 1 | 1.0 | 1.0 | 150 | 150 | 20 | 120 | 60 | 30 | 3 | HH | 57 | HH | NA | 2 | 1 |
| 8 | Michikichi | mikungu | 5 | 1.0 | 20.0 | 400 | 8,000 | 30 | 5,600 | 45 | 2,000 | 167 | 15,212 | 8,366 | HH | 608 | 30 | 15 |
| 9 | Mimaleya | pieces | 1 | 1 | 100 | 5 | 500 | 10 | 450 | 45 | 225 | 19 | HH | 1,000 | HH | 40 | HH | 1 |
| 10 | Viazi vikuu | kilograms | 1 | 1 | 0.8 | 100 | 80 | 15 | 68 | 20 | 52 | 4 | HH | 37 | HH | 7 | HH | 1 |
| 11 | Mifenesi | idadi | 5 | 1 | 200 | 5 | 1,000 | 25 | 750 | 25 | 500 | 42 | 2,433 | 1,460 | HH | 97 | HH | 3 |
| 12 | Miembe | idadi | 10 | 1 | 2000 | 4.5 | 9,000 | 30 | 6,300 | 45 | 2,250 | 188 | 18,250 | 11,000 | HH | 730 | HH | 18 |
| 13 | Minazi | idadi | 10 | 4 | 240 | 50 | 12,000 | 40 | 7,200 | 50 | 1,200 | 100 | 23,750 | 14,250 | HH | 950 | HH | 23 |
| 14 | Milimao | idadi | 5 | 1 | 400 | 1.5 | 600 | 20 | 480 | 55 | 150 | 13 | HH | 667 | HH | 26 | HH | 1 |
| 15 | Michungwa | idadi | 5 | 1 | 500 | 3 | 1,500 | 20 | 1,200 | 40 | 600 | 50 | HH | 2,671 | HH | 106 | HH | 3 |
| 16 | Mikweme | idadi | 2 | 1 | 600 | 5 | 3,000 | 30 | 2,100 | 40 | 900 | 75 | HH | 1,697 | HH | 68 | HH | 2 |
| 17 | Mipapai | idadi | 2 | | 20 | 50 | 1,000 | 10 | 900 | 50 | 400 | 33 | HH | 1,110 | HH | 45 | HH | 1 |
| 18 | Mikarakarat | idadi | 1 | | 2500 | 2 | 5,000 | 40 | 3,000 | 40 | 1,000 | 83 | 1,886 | 1,130 | HH | 75 | HH | 2 |
| 19 | Mipera | idadi | 4 | 1 | 3750 | 2 | 7,500 | 35 | 4,875 | 45 | 1,500 | 125 | 5,444 | 3,266 | HH | 217 | HH | 5 |
| 20 | Miparachichi | idadi | 5 | 1 | 240 | 50 | 12,000 | 30 | 8,400 | 45 | 3,000 | 250 | 13,350 | 6,675 | HH | 534 | HH | 13 |
| 21 | Miwa | idadi | 1 | 1 | 10 | 200 | 2,000 | 20 | 1,600 | 40 | 800 | 67 | 770 | 31 | HH | 31 | HH | 1 |

**KIAMBATISHO 2**

**USHOROBA WA DEREMA: JUMLA YA MALIPO YA FIDIA YALIYOREKEBISHWA KWA MAZAO YOTE, KIJIJI HADI KIJIJI.**

**(HAKUNA FIDIA YA MFUMUKO WA BEI WA MWAKA 2003 – 2006)**

| ZAO | KISIWANI | KAMBAI | KWEZITU | KWEMDIMU | MSASA IBC | JUMLA KWA ZAO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| ILIKI | 4,610,910 | 6,025,191 | 356,439,969 | 445,802,740 | 1,230,348,512 | 2,043,227,322 |
| PILIPILI MANGA | 1,319,975 | 186 | 103,465 | 1,572,243 | 2,492,447 | 5,488,316 |
| KARAFUU | 1,003,200 | 685,140 | 6,289,940 | 1,406,260 | 72,571,626 | 81,956,166 |
| MDALASINI | 96,242 | 2,300 | 321,747 | 143,959 | 3,655,427 | 4,219,675 |
| PARACHICHI | 117,480 | 15,456 | 1,198,872 | 64,535 | 3,445,390 | 4,841,733 |
| MIGOMBA | 3,3351,270 | 200,021 | 12,983,802 | 9,108,422 | 84,669,044 | 110,312,559 |
| MINAZI | 0 | 0 | 1,900 | 199,546 | 28,050 | 229,496 |
| VIAZI VIKUU | 50,562 | 8,821 | 948,622 | 136,312 | 2,446,925 | 3,591,243 |
| KAHAWA | 289,745 | 110,930 | 2,486,354 | 515,872 | 11,082,512 | 14,485,413 |
| MAPERA | 148,644 | 7,553 | 1,280 | 6,749 | 66,913 | 231,139 |
| MIFENESI | 122,815 | 34,698 | 59,284 | 361,235 | 856,515 | 1,434,547 |
| KWEME | 240 | 5,091 | 19,415 | 3,462 | 76,047 | 104,255 |
| MIMALEYA | 3,920 | 0 | 0 | 0 | 432, 409 | 436,329 |
| MIEMBE | 142,220 | 85,030 | 35,773 | 511,272 | 289,526 | 1,063,821 |
| MICHIKICHI | 794,711 | 167,590 | 42,475 | 1,230,751 | 300,459 | 2,435, 986 |
| MICHUNGWA | 318 | 0 | 98,594 | 18,649 | 69,297 | 176,858 |
| MIKARAKARA | 0 | 0 | 150 | 0 | 1,296 | 1,446 |
| MIPAPAI | 2,400 | 0 | 0 | 2,445 | 1,136 | 5,981 |
| MINANASI | 139 | 0 | 13,276 | 5,895 | 14,439 | 33,749 |
| MIWA | 620 | 0 | 6,214 | 19,074 | 4,577,866 | 4,603,774 |
| **JUMLA ZA VIJIJI** | **12,073,560** | **7,348,449** | **381,083659** | **461,117,967** | **1,417,446,822** | **2,279,070,457** |

# RASIMU

## KIAMBATISHO 3

### SAMPULI ZA ORODHA ZA MAZAO

### (MAJINA YA WAKULIMA YAMEHIFADHIWA)

### KUTOKA ORODHA ZA *PROPER CONSULT, 2002*

| JINA LA MKULIMA | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| KITONGOJI: IBC-JUU | | | | | | |
| NA. | JINA LA ZAO | KIWANGO | WINGI | KIASI CHA BEI ? | KIASI KAMILI? | MAELEZO |
| 1 | Iliki | DOS | 520 | 51.00 | 26,520.00 | SHAMBA JIPYA |
| 2 | Ndizi | M | 50 | 3,080.00 | 154,000.00 | |
| 3 | Parachichi | DOS | 50 | 13.00 | 650.00 | |
| 4 | Mdalasini | DOS | 400 | 2.00 | 800.00 | |
| | JUMLA | | | | 181,970.00 | |

| JINA LA MKULIMA | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| KITONGOJI: MAJENGO | | | | | | |
| NA. | JINA LA ZAO | KIWANGO | WINGI | KIASI CHA BEI | KIASI KAMILI? | MAELEZO |
| 1 | Iliki | M | 655 | 5,100.00 | 3,340,500.00 | LIMETUNZWA VIZURI |
| 2 | Ndizi | M | 50 | 3,920.00 | 196,000.00 | |
| 3 | Viazi Vikuu | S | 200 | 7.00 | 1,400.00 | |
| | JUMLA | | | | 3,537,900.00 | |

| JINA LA MKULIMA | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| KITONGOJI: MAGODA | | | | | | |
| NA. | JINA LA ZAO | KIWANGO | WINGI | KIASI CHA BEI ? | KIASI KAMILI? | MAELEZO |
| 1 | Iliki | S | 50 | 204.00 | 10,200.00 | LIMETUNZWA VIZURI |
| 2 | Iliki | M | 87 | 5,100.00 | 443,700.00 | |
| 3 | Iliki | DOS | 120 | 51.00 | 6,120.00 | |
| 4 | Ndizi | M | 13 | 3,080.00 | 40,040.00 | |
| 5 | Ndizi | S | 19 | 224.00 | 4,256.00 | |
| 6 | Ndizi | S | 70 | 7.00 | 490.00 | |
| 7 | Parachichi | M | 1 | 6,675.00 | 6,675.00 | |
| | JUMLA | | | | 511,481,00 | |

## KIAMBATISHO 4

## ORODHA YA WATU WALIOOMBWA KUTOA TAARIFA

**Dar es Salaam**

- **Wizara ya Maliasili na Utalii**

  Felix Mallya, Mratibu, Mradi wa Hifadhi na Usimamizi wa Misitu Tanzania (Tanzania Forest Conservation and Management Project)

  Evariste Nashanda, Meneja, Mradi wa Msitu wa Tao la Mashariki (Eastern Arc Forestry Project (GEF))

  Mathias J. Lema, Meneja, Regional, Catchment, Tanga, Mkoa wa Tanga

  Dkt. Neil Burgess,Mshauri wa Kisayansi, Mradi wa Msitu wa Tao la Mashariki (UNDP-GEF)

- **Wizara ya Ardhi**

  Albert Mallya, Mshauri wa Kisheria

- **Proper Consult (Washauri juu tathmini ya mazao ya Derema, 2002)**

  Bw. Alec R. D. Rwongezibwa, FRS, MBA, Mtathmini wa Mashamba, EMACK (T) Ltd.

- **Ubalozi wa Ufini**

  Veli Juola, (Kansela anayemaliza muda wake (Misitu))

- **Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

  Prof. Goerge Jambiya, Idara ya Jiografia, CKDSM, na Afisa wa Sera, WWF, Tanzania.

  Iddi Mwanyoka, Afisa Mipango, Rasilimali Maji

- **Benki ya Dunia**

  Christian Albert Peter, Mtaalamu Mwandamizi, Misitu

- **Mkoa wa Tanga**

  Bibi Gertrude K. Mpaka, Mkuu wa Mkoa

  Bw. Gervas Msanga, Katibu Mtendaji wa Mkoa

  Bw. Ndihalema Kisheru, Katibu Tawala wa Mkoa

- **Uongozi wa Wilaya, Muheza**

Bibi Joyce Mgana, Mkuu wa Wilaya

Bw. M.T. Mujibhila, Katibu Tawala wa Wilaya

Bw.Obed J. Mwasha, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya

Bw. Mzo, Afisa Tawala wa Wilaya

Bw. M. Mussa, Afisa Mazao wa Wilaya

- **Hifadhi ya Mazingira ya Amani**

  Cordius T. Save, Afisa Mwangalizi, HIMAA

  Mathaya Mbanga Mathew, Mkurugenzi, Utalii, Utafiti na Mafunzo, HIMAA

- **Vijiji vya Ushoroba wa Derema**

  Wenyeviti na Maafisa wengine wa vijiji vifuatavyo, ambavyo viliathirika:

| | | |
|---|---|---|
| Kisiwani | Msasa IBC | Kwemdimu |
| Kwezitu | Kambai | |

- **Wilaya ya Lushoto**

  Bw. E. Mbara, Afisa Ardhi, Lushoto

**RASIMU**

## KIAMBATISHO 5

## RATIBA YA SAFARI ZA USHAURI

| | | |
|---|---|---|
| 25 | Mei, 2006 | Kuwasili Dar es Salaam |
| 26-31 | Mei, 2006 | Kukutana na maafisa wa FBD, maafisa wengine Watanzania, wafadhili na wadau wengine wa Ushoroba wa Derema. |
| 1-7 | Juni, 2006 | Kazi ya Uwandani katika vijiji vya Derema, na Makao Makuu ya Mkoa na Wilaya, Tanga |
| | 1Juni | Mkoa wa Tanga – Kukutana na Afisa Tawala wa Mkoa na TFCMP |
| | 2Juni | Wilaya ya Muheza – Kukutana na Katibu Tawala wa Wilaya |
| | 3Juni | Mkutano – Kijiji cha Kisiwani |
| | 4Juni | Mkutano – Kijiji cha Kwemdimu |
| | 5Juni | Wilaya ya Muheza – Kukutana na Katibu Tawala wa Wilaya, maafisa wa Mazao na Ardhi kutembelea maeneo yenye ardhi ya Msozwe na Mkwajuni |
| | 6Juni | Mkutano – Vijiji vya Msasa IBC na Kwezitu |
| | 7Juni | Mkutano – Kijiji cha Kambai |
| 8-28 Juni, 2006 | | Kuandika Ripoti, Dar es Salaam |
| 29 Juni, 2006 | | Kuhudhurisha Matokeo katika Warsha IBD, Ivory Room DSM |
| 30 Juni, 2006 | | Kuondoka Dar es Salaam |
| 6-13 Julai, 2006 | | Kujadili matokeo ya ripoti na maafisa wa Benki ya Dunia, kasha kuirekebisha ripoti |